

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 21 Desemba, 2013

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (*Mhe. Anna S. Makinda*) Alisoma Dua

MUSWADA WA SHERIA WA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushuru
wa Bidhaa wa Mwaka 2013 (*The Excise Management
and Tarriff (Amendment) Bill, 2013*)**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

*(Muswada Uliotajwa hapo juu Ulisomwa Bungeni
kwa Mara ya Kwanza)*

MUSWADA BINAFSI WA MBUNGE

**Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa wa
Mwaka 2013**

(Kusomwa mara ya Kwanza)

*(Muswada Uliotajwa hapo juu Ulisomwa Bungeni
kwa Mara ya Kwanza)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada Binafsi
wa Mheshimiwa Zitto Kabwe, sasa utaanza kuwepo kwenye
Website ya Bunge na utakuwa *public* mpaka
utakapopangiwa tarehe ya kujadiliwa na utapelekwa
kwenye Kamati zitakazohusika wakati mwafaka.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI

*Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushuru
wa Bidhaa wa Mwaka 2013 (The Excise Management and
Tariff) (Amendment) Bill, 2013*

(Kusomwa Mara ya Pilli)

ISSN 0856-035X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BILL SUPPLEMENT

No. 17

13th December, 2013

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.
50 Vol. 94 dated 13th December, 2013*

Printed by the Government Printer, Dodoma by
Order of the Government

**THE EXCISE (MANAGEMENT AND TARIFF)(AMENDMENT)
ACT, 2013**

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Sections *Title*

- | | |
|----|---------------------------|
| 1. | Construction. |
| 2. | Amendment of section 124. |
| 3. | Amendment of section 125. |

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,
13th December, 2013

OMBENI Y. SEFUE
Secretary to the Cabinet

A BILL

for

An Act to amend the Excise (Management and Tariff) Act.

ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania.

Construction
Cap.147

1. This Act may be cited as the Excise (Management and Tariff)(Amendment) Act, 2013 and shall be read as one with the Excise (Management and Tariff) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of
section 124

2. The principal Act is amended in section 124 by-

- (a) deleting figure "14.5" appearing in subsection (3) and substituting for it figure "17"; and
- (b) deleting subsection (6C).

Amendment of
section 125

3. The principal Act is amended in section 125(1) by-

- (a) inserting the phrase "or any device used to facilitate electronic communication" between the words "phone" and "is" appearing in paragraph (d);
- (b) deleting a semi colon appearing in

paragraph (f) and substituting for it a full stop; and
(c) deleting paragraph (g).

OBJECTS AND REASONS

The Bill proposes to amend the Excise (Management and Tariff) Act, (Cap.147) for purposes of enabling the effective implementation and realization of the objectives of such law. The amendments are aimed at accommodating economic and technological updates that are influencing the national economy and social needs of the society.

The Bill proposes to amend the Excise (Management and Tariff) Act, (Cap.147); whereby section 124(3) is amended by increasing the excise duty imposed on telecommunication services from the rate of 14.5% to the rate of 17% on the dutiable value. This Part also proposes to delete subsection (6C) because the collection of excise duty on telecommunication sim card under that subsection has proved difficult to realise. This Part also proposes amendment to section 125(1) to include, in addition to mobile phone, any service used to facilitate electronic communication or transmission of data to attract duty.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwa madhumuni ya kuwezesha matumizi ya Sheria hii yafanywe kwa uhakika na kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Marekebisho haya yana lengo la kurekebisha Sheria hii ili iendane na mabadiliko mbalimbali ya kiteknolojia na kiuchumi ambayo yamejitokeza katika miaka ya hivi karibuni na yana athari katika uchumi wa Taifa na mahitaji ya wananchi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, (Sura ya 147), ambapo kifungu cha 124 kinafanyiwa marekebisho kwa lengo la kuongeza ushuru kwenye huduma za mawasiliano ya kielektroniki kutoka kiwango cha asilimia kumi na nne nukta tano (14.5%) hadi kumi na saba (17%), pia inapendekezwa kufuta kifungu kidogo cha (6C) kwa kuwa ukusanyaji wa kodi ya simu chini ya kifungu hicho kidogo umekuwa ni mgumu kutekelezeka. Sehemu hii pia inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 125(1) kwa kuongeza, pamoja na simu za mikononi, huduma nyingine zinazowezesha mawasiliano ya kielektroniki au usambazaji wa data kutozwa kodi.

Dodoma,
13 Desemba, 2013

WILLIAM AUGUSTAO MGIMWA
Waziri wa Fedha

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa wa Mwaka 2013 (*The Excise Management and Tariff (Amendment) Act, 2013*).

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha, Namba Nne ya Mwaka 2013 kwa lengo la kuwezesha utekelezaji bora wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri wakati Kamati ilipokutana Mjini Dodoma, tarehe 20 Desemba, 2013. Vilevile nawashukuru wadau mbalimbali, ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakitoa ushauri na mapendekezo, ambayo Serikali imeyazingatia katika Muswada huo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)]

Kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuwashukuru Mheshimiwa William Mgimwa - Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa - Waziri wa Masiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Janeth Mbene - Naibu Waziri mwenzangu na Mheshimiwa Jaji Fredrick Werema - Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Fedha na hususan Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa juhudini zao za kufanikisha maandalizi ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mojawapo ya hatua za kupanua wigo wa mapato zilizochukuliwa na Serikali ili kuongeza mapato yake katika mwaka 2013/2014, ilikuwa ni kutoza ushuru wa bidhaa kwenye kadi za simu wa kiasi cha shillingi 1,000 kwa mwezi kwa kila kadi. Hatua hiyo ilitarajiwani kuipatia Serikali mapato ya shillingi 178,000,414 yaliyopangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maji pamoja na Umeme Vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya Sheria hii kupitishwa na Bunge, utekelezaji wake ulianza. Hata hivyo, wakati Serikali inajiaandaa kukusanya ushuru huu, kampuni za simu na watumiaji wa huduma, walipinga utekelezaji wake kuititia Vyombo vya Sheria. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta husika, ilifanya uchambuzi wa kina na kutafuta namna bora ya kukusanya kodi hii. Hivyo basi, mapendekezo tunayowasilisha yatawezesha kodi hii kukusanya bila ya usumbufu wowote.

Mheshimiwa Spika, naomba kusitiza kuwa, mapato yanayotokana na kodi hii hayajabadiishwa matumizi yake ya kugharamia huduma za maji na umeme vijijini kama ilivyopitishwa katika Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2013/2014. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwa kufuta kodi ya ushuru wa shillingi 1,000 kwa *sim card* kwa kila mwezi ili kufidia pengo la mapato.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)]

Serikali inatarajia kupata bilioni 148 kutokana na kufutwa kwa kodi hii. Sheria zinazobadilishwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupandisha kiwango cha ushuru huo wa huduma za mawasiliano kutoka asilimia 14.5 hadi asilimia 17. Utaratibu huu unaopendekezwa utamwezesha kila mtumiaji wa huduma za mawasiliano kulipa ushuru unaolingana na matumizi yake. Hivyo, mtu atakayetumia kidogo atalipa kidogo na mtu anayetumia zaidi atalipa zaidi tofauti na mfumo wa kulipa kiwango kimoja pasipo kuzingatia kiasi cha matumizi.

(ii) Kupanua wigo wa kutoza ushuru huo kwa kujumuisha huduma zote za mawasiliano ya *ki-electronic* (*Electronic Communication Services*), huduma za kusafirisha mawasiliano kwa njia ya waya (*Optical Fibre*), njia zisizotumia *wire* na teknolojia nyingine yoyote ya aina hiyo, huduma za usambazaji wa mitandao, huduma za kusafirisha *data*, huduma za nukushi na huduma nyingine za *ki-electronic* za namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, hatua zote mbili zinatarajia kuipatia Serikali kiasi cha shilingi bilioni 148. Aidha, shilingi bilioni 30 zitalipwa na makampuni ya simu ili kukamilisha makadirio ya mapato ya ushuru wa huduma za mawasiliano katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Fedha hizi zote zinakusudiwa kukamilisha mafungu ya bajeti yallyopitishwa katika Wizara za Maji pamoja na Wizara zinazoshughulikia umeme.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na changamoto zilizojitokeza, Serikali itaendelea kuangalia namna bora ya kuongeza mapato ya ndani katika bajeti ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu una sehemu moja, Ibara ya (1) inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la Sheria.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya (2) ya Muswada

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)]

inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 124, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, kwa kufuta asilimia 14.5 na badala yake kuweka asilimia 17. Lengo la mapendekezo haya ni kuongeza ushuru kwenye huduma za mawasiliano ya ki-electronic kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 14.5 hadi 17. Aidha, Ibara hii inapendekeza pia kufuta kifungu kidogo cha 6(c) kinachohusiana na kodi ya shilingi 1,000 kwa kila kadi ya simu kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya (3) ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 125(1) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwa kuongeza pamoja na simu za mkononi, huduma nyingine zinazowezesha mawasiliano ya ki-electronic au usambazaji wa data kutozwa kodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu na hatimaye kuupitisha kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, asubuhi ya leo, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2013, ili niweze kutoa Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ya Mwaka 2013 (*The Excise (Management and Tariff) (Amendment) Act, 2013*).

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

Mheshimiwa Spika, kwa heshima, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ya Mwaka 2013 (*The Excise (Management and Tariff) (Amendment) Act, 2013*), iliyowasilishwa na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum - Kaimu Waziri wa Fedha, hivi punde wakati akiwasilisha Hoja ya Serikali kuhusu Muswada huu.

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha Namba 4 ya Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya marekebisho haya ni kuweka utaratibu utakaowezesha utekelezaji bora wa Sheria hiyo na hivyo kuiwezesha Serikali kutoza na kukusanya kwa uhakika ushuru wa bidhaa kwenye kadi za simu (*SIM Card*) kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mojawapo ya hatua za mapato mapya zilitopendekezwa na Serikali kuititia Muswada wa Sheria ya Fedha kwa huu wa Fedha (2013/2014), ilikuwa kuanzisha ushuru wa bidhaa wa shilingi 1,000 kwa mwezi kwa wamiliki wa simu za mkononi ambao utakusanya na Kampuni za Simu kwa niaba ya Serikali. Hatua hiyo ilitarajiwa kuipatia Serikali mapato ya shilingi 178.4 billioni ili kugharamia Miradi ya Maji na Umeme Vijijini. Aidha, hatua hii illengwa kuwafikia Wananchi wengi zaidi katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa wigo wetu wa mapato kwa sasa bado ni mdogo na hatujaweza kufikia kikamilifu sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa na mtoa hoja, tangu Bunge lako Tukufu liridhie kuanzishwa kwa ushuru huu wa bidhaa kwenye kadi za simu, utekelezaji wa Sheria hii umeonekana kuwa na ugumu hususan katika ukusanyaji wa kodi hiyo. Sheria kama ilivyo, inataka kodi hiyo ikusanywe na kampuni za simu kwa niaba ya Serikali kila mwisho wa mwezi. Hali hii imeleta ugumu katika ukusanyaji kutohana na ukweli kwamba, baadhi ya Wananchi wetu wanaomiliki

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

kadi za simu, matumizi yao hayafikii kiwango cha shilingi 1,000 kwa mwezi, kilichowekwa na sheria. Aidha, kodi hii pia imeonekana kutokuwa na usawa, katika misingi ya kodi hili suala ni muhimu sana kwa watumiaji wa simu kwa kuwa haitozwi kulingana na matumizi ya mmiliki wa simu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kupata suluhisho la kuwezesha kodi hiyo iweze kukusanya kama ilivyokusudiwa, Kamati ya Bajeti imekutana kwa nyakati tofauti na Uongozi wa Wizara ya Fedha pamoja na Maofisa Watendaji wote wa Kampuni za Simu hapa nchini.

Jitihada za Kamati ya Bajeti za kuwakutanisha wadau, yaani Kampuni za Simu na Serikali, ndizo zimewezesha kupatikana kwa muafaka kati ya Serikali na Kampuni za Simu juu ya suala hili zilizopelekea Serikali kuwasilisha Muswada huu leo asubuhi hii. Muswada huu unakusudia kufuta ushuru wa shilingi 1,000 kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Sheria husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ili kufidia pengo litakalotokana na kufutwa kwa kodi hii, Muswada ulioletwa na Serikali unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa katika huduma za mawasiliano unaotozwa kuititia sheria hii ili kuboresha ukusanyaji wake. Kuititia Muswada huu inapendekezwa:-

(i) Kupandisha kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa huduma za mawasiliano kutoka asilimia 14.5 ilivyo sasa hadi asilimia 17.

(ii) Kupanua wigo wa kutoza ushuru huo kwa kujumuisha huduma zote za mawasiliano ya kielektroniki zikijumuisha telefax, simu za mezani, *pager* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inawashukuru sana Naibu Mawaziri wa Fedha; Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (Mb) na Janeth Mbene (Mb), Katibu Mkuu Wizara ya Fedha - Dkt. Likwelile, pamoja na Wataalam wa wizara hiyo, ambao mara kwa mara wameshirikiana na Kamati katika kutafuta

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

ufumbuzi wa changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sheria inayofanyiwa marekebisho leo. Aidha, Kamati inatambua na kupongeza kwa dhati, ushirikiano wa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia - Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa kwa ufanuzi wa kina na ushauri alioutoa katika kutafuta ufumbuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa, Mabadiliko ya Sheria yanayopendekezwa hayatarajiwi kuathiri mapato ya Serikali ambayo yalikusudiwa kukusanya kutokana na kodi hii, yaani shilingi 178.4 bilioni. Hatua hii mpya ya kodi inayopendekezwa na Serikali, inatarajia kuipatia Serikali mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 148.4 katika kipindi cha kuanzia Januari 1 hadi Juni 30, 2014. Tofauti iliyobakia kama alivyoeleza mtoa hoja, itafidiwa na Kampuni za Simu katika utaratibu ambao Serikali na kampuni hizo wamekubaliana.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unalenga kuweka usawa katika utozwaji wa kodi katika eneo hili la simu kwa kuwa sasa kodi iliyopendekezwa itatozwa kulingana na matumizi ya simu na mmiliki wa *SIM CARD*. Kwa mantiki hii, azma iliyokuwepo hapo awali ya kuwashirikisha Wananchi katika kuchangia maendeleo yao wenyewe, itaendelea kutekelezeka bila kuwapa mzigo mkubwa zaidi watumiaji wadogo kama ilivyokuwa awali. Kamati inapongeza Serikali kwa hatua hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unakusudia kupanua wigo wa utozaji wa ushuru wa bidhaa kwa kujumuisha huduma zote za mawasiliano ya kieletroniki (*Electronic Communication Services*), kama vile *data, pager, telefax, simu za mezani na mengine*. Hii ina maana kwamba, sehemu ya kodi iliyokuwa ilipwe na kampuni za simu pekee, sasa itachangiwa pia na kampuni zingine za mawasiliano. Kamati inaafiki uamuzi huu na inaishauri Serikali kuendelea kupanua wigo wa kodi katika maeneo mengine kwa lengo la kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika pamoja na nia njema ya Serikali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

ya kuleta Muswada huu, Kamati inashauri kuwa, hatua zilizopendekezwa ziangaliwe upya katika Bajeti ya mwaka ujao wa fedha, kwa lengo la kuziboresha kwa kupunguza kiwango cha kodi hiyo kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 17 angalau hadi asilimia 12 kama ilivyo katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua hii, Kamati inaamini, itachochea matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kufikiwa kwa mapendekezo yaliyoletwa na Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu, ni matokeo ya makubaliano baina ya wadau husika, yaani Kamati ya Bajeti na Serikali. Makubaliano haya yalifikiwa kwa kuzingatia masilahi ya nchi bila shinikizo kutoka upande wowote. Hata hivyo, kwa madhumuni ya uendeshaji bora wa shughuli za Serikali, hasa katika utungaji wa sheria za kukusanya mapato, Kamati ya Bajeti inashauri kuwa ni vyema Serikali ikawa inafanya mawasiliano na wadau wote wanaoguswa na mapendekezo ya kodi yanayokusudiwa kufanya na Serikali, ikiwa ni pamoja na Wizara inayoguswa na kodi husika. Kufanya hivi kutaondoa migongano isiyo ya lazima ambayo inaweza kujitokeza katika ukusanya wa kodi husika. Ni matumaini ya Kamati kuwa, iwapo ushauri huu utazingatiwa, Serikali itaepuka migogoro na mashauri ya kesi za kodi yasiyo na ulazima.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa mara nyine, kwa kunipa fursa hii niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda kuwashukuru kwa dhati tena, Naibu Mawaziri Wizara ya Fedha na Wataalamu wao, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wadau wote, kwa kushirikiana vyema na Kamati katika kuufanya kazi Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu mabadiliko ya Sheria hii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Andrew J. Chenge – Mwenyekiti, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour – Mjumbe, Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami – Mjumbe, Mheshimiwa Mansour Shaniff Hiran – Mjumbe, Mheshimiwa Josephat Kandege – Mjumbe, Mheshimiwa Christina M. Lissu – Mjumbe, Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu – Mjumbe, Mheshimiwa James F. Mbatia – Mjumbe, Mheshimiwa Assumper Mshama – Mjumbe, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed – Mjumbe, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh – Mjumbe, Mheshimiwa Joseph R. Selasini – Mjumbe, Mheshimiwa Saleh Pamba – Mjumbe, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu – Mjumbe, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo – Mjumbe, Mheshimiwa Ritha Mlaki – Mjumbe, Mheshimiwa Peter Serukamba – Mjumbe na Mheshimiwa John M. Cheyo – Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge letu – Dkt. Thomas Kashililah na Watumishi wote wa Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati, kwa kuihudumia vyema Kamati hadi kukamilisha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Bunge lako Tukufu, lijadili mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali kupitia Muswada huu na hatimaye liweze kuyaafiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Bajeti na ninapenda kutamka kuwa, ninaunga mkono hoja hii.
(Makof)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Msemaji kutoka Upande wa Upinzani, aliyehusika na Muswada huu. Mheshimiwa Christina Mughwai!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Kabwe Zitto, naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa (*The Excise Management and Tariff (Amendment) Act of 2013*) na hii ni kwa Mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeleta Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kama ilivyokuwa imepitishwa na Bunge hili hapo mwezi wa Juni, 2013. Muswada huu unapendekeza Kifungu cha (2) kufanya marekebisho Kifungu cha (124) cha Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli uliowazi kuwa, upitishwaji wa Muswada wa Fedha wa Mwaka 2013, ulipitishwa pasipo kuzingatia Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuwa zilifanyika njama hususani kuvizia, kwani ni ukweli kwamba, Waheshimiwa Wabunge wengi hawakupata nafasi ya kujadili kwa kina. Hii ilitokana na ukweli kwamba ... (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, umesema ni nani aliyevizia? Sijaelewa ni nani aliyefanya hiyo kazi kwa sababu katika Bunge hilo halistahili kusemwa. Ni nani aliyemvizia mwingine; ni Kamati ya Bunge ya Bajeti au ni nani? (*Makofii*)

MHE. CHRISTINA L. MUGWAI - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ni Serikali. Ninamalizia inaelezewa katika hii *paragraph*.

SPIKA: Maneno mengine mazito hapa siyo mahali pake. (*Makofii*)

Hapana. Waheshimiwa Wabunge, tusizungumze, tunatunga Sheria hatutungi majungu hapa. Hamuwezi kuingiza maneno ambayo mimi siyaelewi. (*Makofii*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI - NAIBU MSEMAJI MKUU
WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:**
Mheshimiwa Spika, ninaomba nirudie hii itaelewaka
paragraph nzima ikiisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa, upitishwaji wa Muswada wa Fedha wa Mwaka 2013, ulipitishwa pasipo kuzingatia Maoni ya Kambi rasmi ya Upinzani, kwa kuwa zilifanyika njama hususani kuvizia, kwani ni ukweli kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi hawakupata nafasi ya kujadili kwa kina. Hii ilitokana na ukweli kwamba, wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya nchi Bungeni, alisema kuwa kodi ya laini za simu haipo kwani iliandikwa kimakosa kwenye Hotuba yake na akaleta *addendum* kwa ajili ya marekebisho hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mazingira yaliyopelekea kifungu kilichofutwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kujitokeza kwenye Jedwali la Marekebisho kwenye Muswada wa Fedha, yalipelekea Waheshimiwa Wabunge wengi kutokuelewa maana hasa ya Serikali kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, Kambi Rasmi ya Upinzani ilioa mapendekezo yake wakati huo kuhusu Sheria hii ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 124 na ninaomba kunukuu mapendekezo hayo:-

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha unapendekeza marekebisho mengine katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, ambayo yatakuwa na athari mbaya na kubwa kwa masilahii ya Wananchi wengi wenye vipato vya chini katika nchi yetu. Kwa mujibu wa mapendekezo haya, huduma za mawasiliano za aina zote, ikiwa ni pamoja na kutuma na kupokea simu au ujumbe wa maneno au sauti au picha, sasa zitatozwa ushuru wa asilimia 14.5, juu ya gharama za sasa za huduma hizo. Nyingi ya huduma za mawasiliano zinazopendekezwa kutozwa ushuru huo wa bidhaa, kama vile *call waiting, call forwarding, caller identification, three way calling, call display, call return, call screen, call blocking, automatic call back, call answer,*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI - NAIBU MSEMAJI MKUU
WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHAJ]

voice mail, voice menus na video conferencing, ni huduma ambazo zimerahisisha mawasiliano kwa wananchi wengi wenye vipato vya chini, na hasa kundi kubwa la vijana. Kwa mapendekezo haya ya Serikali hii ya CCM, huduma hizi ambazo zinapendwa na watumiaji wengi hasa vijana kwa sababu ya urahisi wa matumizi yake, sasa zitatozwa ushuru wa asilimia 14.5. Ninaendelea kunukuu.

"Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba, kwa sababu ya upungufu wa kisheria uliopo sasa, makampuni ya simu yamekuwa yakilipia ushuru wa kupiga na kupokea simu tu, wakati makampuni haya yakiptata mapato makubwa kutokana na simu za mawasiliano ambazo hazitozwi kodi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaelewa haja ya huduma za mawasiliano kuchangia ipasavyo katika mapato ya Serikali, kwa kupanua wilgo wa huduma za mawasiliano zinazotozwa kodi. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiko tayari kuunga mkono Marekebisho ya Sheria ambayo pamoja na kuongeza mapato ya Serikali, yataongeza mzigo wa kodi kwa wananchi wa kawaida wa Tanzania ambao tayari wameelemewa na mzigo mkubwa wa hali ngumu ya masiha, vipato vya chini na umaskini mkubwa.

Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ihakikishe kwamba, ushuru wa huduma za mawasiliano unaopendekezwa kwenye Muswada huu, hautaongeza gharama za matumizi ya simu ambazo tayari ni kubwa sana. Hilo linawezekana kwa Muswada huu kuwa na kifungu kitakachokataza makampuni ya simu kuhamishia gharama za ushuru wa bidhaa, ushuru wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji wa huduma hizo na hivyo kuongeza gharama za matumizi ya simu." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa, Kambi Rasmi ilipinga kuongeza ushuru kutoka asilimia 12 hadi 14.5. Sasa Muswada huu ambao umeletwa kwa Hati ya Dharura, unaongeza ushuru huo kutoka asilimia 14.5 hadi asilimia 17. Ni ushuru huu unaoongezeka tena na ongezeko hili linaenda

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI - NAIBU MSEMAJI MKUU
WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA]

kwa watumiaji na siyo kwa wamiliki wa makampuni ya simu.
(Makofii)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kukubaliana na ushauri ambao tuliutoa tarehe 27 Juni, 2013, kama nilivyonukuu hapo juu. Aidha, kuhusu kufutwa kwa Kifungu cha 6(c) kinachoongezwa, kinachotaka kutozwa ushuru wa *line* za simu kwenye Sheria hii, Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono kufutwa kwa kifungu hiki cha kodi katika *line* za simu kwani kitawezwa kuondolea Wananchi wa kipato cha chini mzigo ambao tayari ni mkubwa katika suala la mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni haya machache, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (Makofii)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunao wachangiaji wengi, lakini jana tulitoa hoja kwamba ifikapo saa sita mchana tunatakiwa tuwe tumemaliza.

Naomba nimwite Mheshimiwa Saleh Pamba, atafuatia Mheshimiwa James Mbatia, atufuatia Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Mheshimiwa Saleh Pamba!

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache katika muswada ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bajeti. Nina-*declare* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, ambayo ilipitia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali, kwa kuliona suala hili na vilevile kuleta marekebisho haya kwa Hati ya Dharura hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niweke mambo sawa hasa kuhusu utaratibu wa kutunga Sheria hapa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SALEH A. PAMBA]

Bungeni. Sheria na Muswada wowote unakuja hapa Bungeni, unapitia katika taratibu zote, vilevile Bunge linakaa kama Kamati na Wabunge wana haki kabisa ya kuleta marekebisho yoyote katika sheria yoyote inayoletwa na Serikali. Kwa hiyo, ninapenda niseme kwamba, Serikali haikuvizia, ililetä Muswada hapa ukajadiliwa wazi na *Finance Bill* ikapitishwa ikawa Sheria ya Kodi kwa Mwaka 2013/2014. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yaliyojitokeza ni katika utekelezaji. Kwa kawaida, Sheria zote zinazotungwa duniani, zinapopelekwa kwenye utekekezaji kama kuna tatizo linatokea katika utekelezaji, Sheria hizo lazima zirekebishwe. Lengo kubwa ni kuhakikisha tunakusanya mapato, Serikali iweze kwenda na tuwaletee Wananchi wetu maendeleo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo ninataka kulizungumzia ni hili ambalo limejitokeza. Ninataka nitoe pendekexo kwa Serikali kwamba, Serikali nao wawe waangalifu; kwa sababu tukifikia mahali ambapo Sheria ya Kodi hasa inayohusu makusanyo, inaanza kuwa *disputed huko*, inaonekana kunakuwa na matatizo katika mchakato mzima wa kufikia kwenye Sheria mbalimbali za Kodi. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ninachoiomba Serikali, najua upo utaratibu mzuri wa kuwahuisha wadau katika kufikia malengo mbalimbali katika ku-*introduce* kodi mbalimbali. Ninaomba kabisa kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwamba, suala hili lipewe kipaumbele, katika kodi yoyote ambayo inapendekezwa, basi wadau wote washirikishwe watoe maoni yao, ili haya yaliyojitokeza katika hasa kodi hii ya simu yasijitokeze tena siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, ninataka nzungumzie suala moja ambalo ni muhimu na Watanzania wanansikia hapa. Nchi zote zile ambazo tunazitungumzia sasa hivi kwamba zimeendelea; Uchina, Ulaya, hizi nchi za Mashariki na kahalika, kuna mambo mawili ambayo yamezfanya nchi hizi ziendelee. La kwanza, Wananchi wote kuwa pamoja na Serikali yao. La pili, ambalo ni la msingi na ni muhimu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SALEH A. PAMBAJ]

kabisa ni Wananchi wale ku-sacrifice kwa ajili ya maendeleo yao. (Makofi)

Madhumuni ya kodi hii, ambayo tulipitisha hapa Bungeni, Serikali haikuwa na madhumuni kwamba, fedha hizi zinaenda kununua magari au kununua ndege ya Rais, hapana. Fedha hizi shilingi bilioni 178, zilikuwa zinarudi kwa Wananchi wenyewe hasa kwa maeneo yanayohusu maji na maeneo yanayohusu umeme vijiji. (Makofi)

Kwa misingi hiyo basi, ni vizuri sisi Wanasiaya, tukachukua nafasi, baada ya kupitisha Sheria hizi Bungeni; ninajua zinawagusa Wananchi wetu na tunajua kwamba, Wananchi wetu ni maskini, lakini ni lazima tufanye *political groundwork* ya kuhakikisha tunawaelimisha Wananchi wetu kuhusu madhumuni ya Sheria hii. Hilo ndiyo ninaona halikuwepo hapa na kukawa na mkanganyiko mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ninataka kuzungumzia ni kwamba, nimefarijika sana na Maoni ya Serikali yaliyoletwa hapa Bungeni kwamba, fedha hizo zitapatikana, hakutakuwa na upungufu katika Bajeti. Ninaipogeza sana Serikali katika hatua hii ambayo wameichukua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni kwamba kodi hii tumeileta mwaka huu. Tumeona matatizo yake. Ukweli ni kwamba, kodi hii ukiilinganisha na nchi za jirani za Afrika ya Mashariki, ni kodi ambayo iko juu sana. Hailingani na jinsi ilivyo katika maeneo mengine Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi. Kwa hiyo, tunawaomba wenzetu wa Serikali, tutapotoka hapa warudi katika *drawing board*, wahakikishe mwakani tunaporudi katika Bajeti, tutafute njia nydingine mbadala ya kupata kodi ambayo haitawaumiza Wananchi wetu, tuweze kusonga mbele katika maendeleo yetu. Kwa hiyo, ninawaomba Serikali hili lilitotokea limetokea, *MOAT* wametoa ushirikiano mkubwa sana kwa Serikali, lakini Serikali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SALEH A. PAMBA]

pia kama nivyosema, irudie kukaa na wadau na kuhakikisha haya yaliyojitokeza hayajitokezi tena.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niyaseme haya na niweke sawa mambo haya, kwa sababu tumeya-*discuss* sana katika Bajeti, na kwamba katika muda karibu wa miezi sita fedha hazikukusanya. Kuanzia Januari fedha hizi zitaanza kupatikana, zitaanza ku-flow, zitakwenda kwa Mheshimiwa Profesa Muhongo pale ili tuweze kuanza kazi za kuwapelekea Wananchi wetu maji na umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Eng. James Mbatia, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchomba!

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, niungane na Maoni ya Kamati ya Bajeti na nimpongeze Mwenyekiti wetu kama alivyowasilisha hapa vizuri, kuhusu Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, *taxation is a compulsory payment to the Government. Compulsory, ni ya lazima kulipwa kwa Serikali ili Serikali ifanye majukumu yake.*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kodi hii ya simu ulianza kwenye Mapendekezo ya Kamati ya *Chenge One*, mwaka 2011, lakini Serikali haikuchukua muda wa kutosha kufanya utafiti kwenye kodi hii. Ilipoletwa kwenye Bunge lako Tukufu na ikapitishwa, inaonekana Serikali haikufanya kazi kwa pamoja kuileta ndani ya Bunge lako Tukufu. Huu ni ushahidi ulio wazi pale Mawaziri ndani ya Serikali, baada ya kuitishwa Muswada ulioletwa na Serikali ndani ya Bunge lako Tukufu, kwenda kwenye Vyombo vya Habari kuupinga Muswada ulioletwa ndani ya Bunge lako Tukufu. Sasa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JAMES F. MBATIA]

uwajibikaji wa pamoja wa Serikali upo wapi? Serikali inapopinga Muswada wake; Waziri anayepinga kwa nini bado yuko kwenye nafasi yake mpaka sasa? (Makof)

Mheshimiwa Spika, labda nishauri tu kwa sababu Mawaziri wengine wameondolewa jana, Baraza lijalo la Mawaziri, wapigwe tena msasa wajue majukumu yao ya kufanya kazi yako vipi. Kwa sababu huwezi ukapitisha Sheria, Serikali ni moja, imepita ndani ya Baraza la Mawaziri, mwenye kutoa kibali cha kodi ni Rais, halafu Waziri anaenda kwenye Vyombo vyta Habari kuupinga Muswada wa Serikali yake! Kwa kiasi kikubwa walioleta mkanganyiko wote huu mpaka leo hii hapa ni Serikali yenyewe. (Makof)

Isitoshe, Serikali hiyo ya Chama cha Mapinduzi, hata kama siyo, na Wabunge hao wa Chama cha Mapinduzi; wewe ni Waziri unatokana na Ubunge wa Chama cha Mapinduzi, Chama chako ndiyo kinachoismamia Serikali, wewe Mbunge wa Chama hicho hicho unakwenda kuipinga Serikali, una haki gani ya kuwepo! *How!* Na ndiyo mmeleta mgogoro mkubwa huu mpaka leo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, pale Serikali inaposhirikiana na Wafanyabiashara wachache kupinga kulipa kodi, mnaleta mgogoro katika Taifa na hii hatuwezi tukaruhusu.

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu tusipokuwa makini, mengine yatajitekeza zaidi. Nasema hivyo kwa sababu *TCRA* imesema *sim card* zilizopo ni milioni 28. Tukakubaliana watakaokatwa kodi hiyo ni asilimia 50 tu na wakatuahidi Desemba, 2011 kwamba, ifikapo Julai, 2013 watakuwa wameshafunga mitambo na itajulikana kama James Mbatia natumia simu ya 200,000 kwa mwezi, nitakatwa zaidi na huyu anayetumia 500 hatakatwa chochote. Inakuwaje tena *TCRA* hiyohiyo iende *public* na ni *Agency* ya Serikali, baada ya Sheria kuitishwa hapa na *TCRA* ikaenda kwenye *public* kusema na sisi tulipinga kodi hiyo na hakuna yeyote ameshachukuliwa hatua ya kinidhamu mpaka leo hii. Ndiyo tunakuwa na mashaka mengi, walakini na walakini, *questions mark* zipo nyingi tu. (Makof)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JAMES F. MBATIA]

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, mkiendelea kufanya kazi kwa misingi hiyo mtaleta mgogoro mkubwa sana; kwa sababu fedha hizi zilitakiwa ziende kwenye umeme vijijini na kwenye maji, sasa tumekaa miezi sita yote hakuna maendeleo yoyote.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe uliishauri Serikali kwamba, waende wakakope fedha mahali ili shughuli za maendeleo zianze kutekelezwa kuanzia mwezi Julai na kodi ikishakusanya irudishwe. Katika mzozo huo, mnatoka hapa Serikali mnaanza kugombana wenyewe kwa wenyewe. Inabidi tuwe wakali zaidi Bunge hili tuweze kuwasimamia Watanzania wapate maendeleo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hao Mawaziri waliomshauri Rais, wafanyabiashara wanamfikia halafu wanasema tangu tarehe 1 Agosti, walangalle tena upya Sheria hii na ye ye ameshaisaini. Kwa kweli hamkumtendea haki Rais ni kumfedhehesha Rais kabisa! Lazima tuwe wakweli na ukweli unauma lakini ni wa Mwenyezi Mungu. Ikulu ni mahali patakatifu; wamefikafikaje wafanyabiashara hawa? Kwa utaratibu upi; na Mawaziri walewale waliopitisha Sheria ndio wanaambatana na hawa wafanyabiashara kwenda kwa Rais! Ebo nchi gani hii? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitoe tu ushauri kwamba, tunapokubaliana na Kamati yako ya *Chenge One* ilifanya kazi nzuri sana, viro vyanzo vingi vya mapato, tukiangalia wenzetu wa Kenya, kwenye simu hizi za kawaida walishaondoa kodi zote tangu mwaka 2009, wao wanaenda kwenye matumizi. Simu zinazouzwa hapa nchini leo hii kila mwezi ni zaidi ya simu 430,000, lakini zinazolipiwa kodi kwa takwimu sahihi ni asilimia kumi tu, yaani ni 43,000. Sasa tunapotoa mawazo kwenye Kamati ya Bajeti na Bunge linatoa mawazo lakini Serikali inashindwa kutekeleza, tunakuwa na wasiwasi mkubwa sana kuwa kulikoni au baadhi ya Viongozi wa Serikali wana hisa kwenye haya makampuni ya simu? Wanakuwa na *conflict of interest?* Unakuwa na hisia za namna hiyo. Kwa namna hii hatutaweza kuendesha nchi!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JAMES F. MBATIA]

Mheshimiwa Spika, wenzetu Uingereza, sasa hivi tupo kwenye *Three G*, walipoenda kwenye *Four G* wameenda kwenye minada, na kutoka kwenye masafa ya *Three G* kwenda *Four G* wamepata *pound billion* 3.9, ambazo ni takribani shilingi triliuni tisa za Tanzania. Inahitaji Sekta ya Mawasiliano, tunapotoka kwenye *Three G* kwenda kwenye *Four G* muwe mmeshaandaa kanuni vizuri na sisi twende kwenye mnada, tusiende tena kwenye leseni za kawaida kwenye makampuni ya simu.

Tuitake Sekta ya Mawasiliano ifanye utafiti wa *Four G* kwenye Nchi Wanachama za Afrika Mashariki na iende nje ya Afrika Mashariki, tuone namna gani Sekta ya Mawasiliano ambayo haijaleta pato la kutosha ndani ya Taifa hili japo imepanuka sana. Kuna ujanjaujanja mwingi unaafanyika ndani ya Sekta ya Mawasiliano tupate fedha kwa ajili ya kuhudumia Taifa la Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi ambayo yatakuja kwenye Bajeti ijayo. Kutokana hili lililotokea, niungane na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bajeti na Mheshimiwa Pamba kwamba, ni vyema Wizara za Kisekta na Hazina, wakakaa pamoja mapema katika *ku-harmonise* mambo haya kwa pamoja. Kwa sababu haiwezekani wakati wa Kamati unamwuliza Waziri huyu anasema mimi sina habari, Waziri mwingine anasema mimi sina habari na ukimwuliza Waziri mwenye dhamana anakwambia nimepata ushauri kutoka huku na siyo kwa Waziri mwenzake, inakuwa haileti picha nzuri.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi kwenye *deep sea* tuna kilomita za mraba zaidi ya 230,000, ambapo 2012/2013 tulishindwa kukusanya zile *loyalty* zaidi ya shilingi bilioni 352. Tunaomba isije tena, mlituambia tupo kwenye mchakato, tunaomba bajeti ijayo Sekta ya Uvuvi iingize mapato kwenye Taifa la Tanzania. Tumeizungumzia zaidi ya miaka miwili sasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia hii ya kadi za simu sasa hivi wanasema labda kwa sababu watu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JAMES F. MBATIA]

wanalipa mapema, *pre-paid* na wanatakiwa kukusanya mwisho wa mwezi, labda utafiti haukufanyika. Je, nikiwaliza wale wa *post-paid* hata kama ni asilimia moja tu mlkusanya kitu gani? Kwa hiyo, kulikuwa hakuna nia njema.

Mheshimiwa Spika, pia tuangalie Sekta nyingi tu kama Sekta za Anga, Sekta za Utalii na kadhalika. Nchi yetu ina vivutio vingi vya utalii, ni nchi ya pili kwa vivutio vya utalii Duniani ukiondoa Brazili, hatujaiangalia ipasavyo Sekta hii. Kwa nini gharama za ndege ya Shirika la Ndege la *KLM* kwa mfano kutoka Amsterdam kuja Dar es Salaam inakuwa ni ghali kuliko kutoka Amsterdam kwenda Nairobi? Ndiyo maana wenzetu wanatuzidi kwenye masuala ya utalii. Kwa nini walipe kodi *KIA* na kwa nini walipe kodi Dar es Salaam? Sasa tupanuke na tuyafanye haya mambo mapema, tushirikiane na maamuzi yanapofanyika na fedha zinapokusanywa, ziende kwenye Sekta husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kodi hizi zitaanza Januari na tumebakwa na miezi sita, nashauri na linawezekana; hizi shilingi bilioni 178.4 mzikope sasa ili ziende kuhudumia maji na umeme vijijini ili mkikusanya mrudishe fedha hizi. Kwa sababu hatuvezi kuendelea kusema tutaendelea kukusanya kaidogokidogo mpaka mwezi wa sita halafu tunaingia kwenye mwaka mwingine wa bajeti; maendeleo yatafanyika saa ngapi? Zikopwe sasa maendeleo yaanze kufanyika kwa sababu uhakika upo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, hizi shilingi bilioni 30 kwenye ushuru ambao ni mkubwa sana wa asilimia 17, tumependekeza waangalie na Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki ambao ni asilimia 12. Kabla ya kwenda kwenye ushuru wa pamoja, tushauriane na Kamati ya Bajeti na Wadau wengine, tuangalie kwenye bajeti ijayo gharamza za simu zishushwe hapa Tanzania ziwe sawasawa na nchi nyingine za Afrika Mashariki. Tukifanya hivyo, tutakuwa tunawatendea haki Watanzania walio wengi na gharama zifanane ili ujanjaujanja wa kukwepa kodi usiwepo. (*Makof*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JAMES F. MBATIA]

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nitumie nafasi hii kukutakia kheri ya Christmas na Mwaka Mpya wewe na Bunge lako Tukufu na Watanzania wote wanaotusikiliza.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwigulu Nchema atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niweke wazi kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na nikiri kwamba, naunga mkono hoja iliyoletwa na Serikali mbele yetu. Naipongeza Serikali kwa kuwa sikuvi. Tunaposema Serikali sikuvi maana halisi huwa ni hii kwamba, Serikali inazingatia malengo na inazingatia Watanzania wanataka nini. Niseme kwamba, Serikali ilipoleta Sheria ya *Sim Card*, lengo lake halikuwa kuwaadhibu Wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba, wakati tunajadili Bajeti ya Wizara ya Maji ni mimi binafsi niliyekuomba utoe maelekezo ya Serikali kuondoa bajeti ile na ikatafute vyanzo mbadala vyta kugharamia maji badala ya kutegemea Miradi ya Benki ya Dunia. Wajumbe wenzetu wanasema, wakati Waziri wa Fedha anawasilisha jambo hili halikuwepo na baadaye likaletwa; ndiyo halikuwepo na likaletwa kwa sababu tuliiagiza Serikali ikatafute vyanzo upya kuliko kutegemea Miradi ya Benki ya Dunia. (*Makof!*)

Niseme tu Wataalamu wetu wametuangusha kwenye hili, kwa sababu wakati tunajadiliana chanzo hiki kipyta kama chanzo cha kodi cha *sim card*, hawakufafanua ugumu huu ambao wamekuja kuufafanua baada ya Sheria kupitishwa. Naendelea kuamini hivyohivyo kwamba, lengo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MWIGULU L. N. MADELU]

Ia kusema kama kuna mtu anatumia shilingi 500,000 kwa mwezi akichangia shilingi 1,000 kwenda kwenye maji bado sioni tatizo lake liko wapi.

Ubaya wa kodi hii waliyotuletea ambayo haikufafanuliwa ilikuwa *flat rate*, ilikuwa inatoza sawasawa kwa kila mtu. Kodi ya aina hiyo mara zote huwa si ya usawa, ni sawasawa lakini si ya usawa. Sasa kutumia mtambo tulitegemea kila mtu atatoa kwa kiwango chake. Kwa hiyo, kwenye hili Serikali si ya kulaumiwa, ilikuwa na nia njema ambayo ililenga kuwapatia Wananchi wake maji na umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hivyo, Serikali imerudi tena, mimi naipongeza kwa hatua hii. Imerudi tena ikiwa na nia ileile ya kutatua tatizo lilitojitekeza, pia kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanatimia ya Wananchi kupata maji. Kwa hiyo, kwa hili naipongeza. Ninashauri jambo moja kwamba, kwa kuwa kodi hii tunayoipitisha sasa, mara nydingi huwa inatumika kama kodi ya ku-*discourage* matumizi ya bidhaa fulani, kodi hii mara nydingi inatumika kwenye bidhaa ambazo hazitakiwi sana zitumike, inatumika ku-*discourage*, ndiyo asili yake ilivyo. Basi Serikali ifidie kwa wakati huu, lakini kule tunakoendelea katika mwaka wa fedha utakaofuata, iangalie mazingira ya kutokuipandisha sana kodi hii, kwa sababu sekta hii ni nyeti kwa maendeleo, ni kiini cha kukua kwa teknolojia. Kwa hiyo, iangalie isije ikatumika kama ambavyo inatumika kwenye sigara, vilevi na mambo mengine ambayo hayapaswi kuendekezwa katika Taifa.

Vilevile Serikali suala ambalo tumekuwa tunaliongelea ambapo ingewekwa na kutumika tusingepata tatizo hili ni mitambo. Kipindi cha nyuma kidogo wakati tunataka kujua Sekta inavyokua, tulipewa takwimu zinazoonesha Watanzania jinsi wanavyotumia simu na tukaambiwa ni moja ya nchi zenye matumizi makubwa tu ya simu. Tulipotaka tupate kipato kutoka kwenye sehemu ile, takwimu zilizokuja zikaonesha kiwango kinachotia huruma sana, ni kama vile idadi ya watu wanaotumia fedha nydingi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MWIGULU L. N. MADELU]

kwenye simu kwa Tanzania ni ndogo sana. Hii ni kwa sababu tunategemea takwimu kutoka kwa watu, kwa hiyo, zinaweza zikatumika kufuatana na masilahi wanayotaka wapate kutokana na takwimu hizo. (*Makofii*)

Serikali ijiridhishe kwa kutilia mkazo suala la mtambo utakaoonesha wanaotumia shilingi 500,000 ni wangapi, wanaotumia shilingi 200,000 ni wangapi na wanaotumia shilingi 1,000 ni wangapi. Suala siyo tu kupata mtambo, lakini pia kupata wataalamu waliofundishwa kutumia mitambo hiyo, kwa sababu mitambo nayo inaweza kutengenezwa kufuatana na mtu anataka kupokea kitu gani.

Niseme jambo moja kwamba, kama Taifa ni vyema sana tukakubaliana kwamba, kulipa kodi kwa kila mtu ni jambo la heshima, kwa sababu ndilo linalotupa heshima ya kujitegemea. Kwa hiyo, tusiendekeze sana mambo ya aina hii ya kuona kama vile jambo la kodi nalo tunaweza tukalipa ama tusilipe, tunaweza kukakaa kujadili na kadhalika. Suala la maendeleo yoyote ni lazima tukubaliane wote kwamba tunatakiwa tufanye wenyewe maendeleo na tusitegemee mtu mwingine.

Niseme mawili tu kwenye hili kwa sababu yana uhusiano na suala la kodi. Watananzia walio wengi hawalipi kodi kufuatana na ziada, wanajibana. Hata wale amba wana biashara na wanaoendelea wanajibana, kwa sababu ni jambo la lazima. Kwa hiyo, ni vyema sana Serikali ikatafsiri kwamba, fedha iliyokusudiwa kwenye maji watu wayaone maji na fedha iliyokusudiwa kwenye umeme watu waone umeme. Hiyo itajenga ari kubwa ya watu kulipa kodi. Tukisema tumepandisha kodi ya mafuta iende kwenye umeme, Wananchi wasipoona umeme, kipindi kingine mtakapowaambia kuhusu kodi hawatakuwa na utayari wa harakaharaka. (*Makofii*)

Vivyo hivyo kwenye hii, tumesema ipandishwe kutoka asilimia 14.5 kwenda asilimia 17 na tukasema iende kwenye maji, ni vyema Wananchi wakayaona hayo maji. Waone tofauti kabla ya kodi hii kupanda na sasa baada

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MWIGULU L. N. MADELU]

ya kodi kupanda. Hicho kitakuwa kichocheo cha kila mtu kuona analazimika na anawajibika kuchangia maendeleo ya nchi yake. Hili ni jambo la kwanza.

Jambo la pili, ni lazima Serikali ibane matumizi. Matumizi ya Serikali yawe kwenye mambo muhimu. Kwa upande wa ukaguzi, tuna udhibiti na ukaguzi. Tunaona zaidi *report* nydingi tunazojadili ni za ukaguzi, tuone na zile za kudhibiti. Tuone Serikali ikidhibiti kwa sababu kukagua tu mambo yanakuwa yalishaharibika, hii sehemu ya udhibiti nayo ichukue nafasi yake. Fedha ambayo imekusudiwa kwenda kwenye eneo fulani iende eneo lilitokusudiwa, matumizi mengine yadhibitiwe. Hili ni jambo ambalo litachochea Wananchi walipe kodi.

Mheshimiwa Spika, siyo tu kwenye Bunge hata Mawizarani, Watanzania wanatakiwa waone hii *element* ya udhibiti na *element* ya matumizi yaliyo bora ya fedha za kodi zao wanazolipa. Mambo mengine yanayojitokeza yanayoonesha Wananchi wanakamuliwa kulipa kodi halafu fedha yao haiendi kwenye maeneo yaliyokusudiwa, ni jambo ambalo halituletei heshima na ni jambo ambalo linakatisha tamaa wale wanaolipa kodi. Hii ifanyike mahali pote, ifanyike Mawizarani, ifanyike kwenye Halmashauri, watu wanapoona Watumishi wa Halmashauri waone fedha inakwenda kule ilikolengwa, itawasaidia wao walipe kodi. Mawizarani watu waone fedha waliyolipa inakwenda kulikokusudiwa na kwa sisi watunga sheria waone fedha ya kodi inakwenda kwenye maeneo yaliyokusudiwa. Yameanza kujitokeza mambo, ukiona fedha inatolewa kwenye eneo fulani na watu wanachukua fedha haifanyiwi kazi, maana yake yale matumizi hayakuwa ya lazima.

Tunapokwenda kwenye bajeti inayofuata, tutumie takwimu za maeneo ambayo hayakufanya vizuri tuondoe fedha zile ziende kwenye maji na umeme. Fedha za Serikali zitumike kwenye mambo ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, mambo haya tusiwarushie tu wengine bali uanze na wewe kwa watu wako hapahapa,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MWIGULU L. N. MADELU]

matumizi kama yale ya kuchukua watu kwenda kufanya burudani Dubai kwa fedha ya Serikali, yanaondoa *morale* ya watu kulipa kodi. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza hili lipo mikononi mwa Spika, mtasema mpaka kufa! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndasa!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami pia nakushukuru binafsi kwa kunipa nafasi nichangie katika Muswada huu ambao umekuja kwa Hati ya Dharura, Muswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa.

Mheshimiwa Spika, kimantiki hakuna ambaye atakataa Serikali kukusanya kodi ambayo madhumuni yake yameelezwa vizuri kwamba, inakwenda kwa ajili ya kusaidia maeneo muhimu ya maji na umeme. Hili halina mjadala na tunakubaliana nalo. Tunauliza tu kwa nini Muswada huu baada ya kuonekana umekuwa mgumu umekaa zaidi ya miezi sita bila kuletwa na kurekebishwa? Hapa tuna mashaka kidogo na lazima mashaka yetu tuyaseme kama ambavyo Mheshimiwa Mbatia alizungumza. (*Makof*)

Tuna wasiwasi kwa sababu kama tutakumbuka, baada ya kupitishwa tu Muswada huu, *MOAT* wamekwenda Mahakamani japokuwa Serikali imeshinda na tunasikia kwamba, hawa jamaa wanataka kwenda katika ngazi za juu za Mahakama. Sasa hapa tunaanza kujiliza; hivi kweli Serikali inashindwa nguvu na makampuni ya simu; kuna nini hapa mpaka wamekubali kulegeza mikono na miguu leo wameleta tena Muswada huu eti tuuridhie?

Mheshimiwa Spika, nina mashaka vilevile kusema kwamba, Muswada huu ulikuwa mgumu kutekelezwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED]

Makampuni ya simu wao walitakiwa wawe mawakala wa kukusanya hii shilingi 1,000, sasa leo wanasema hawana uwezo wa kukusanya; *is it sense?* Wanapataje wao faida? Wanawezaje kuniletea *message* ya kuniambia piga namba hii uchizike, leo waseme wao wanashindwa kukusanya kodi hii na Serikali nayo imeridhia? Hivi ni kitu gani kilicho juu hapa; ni makampuni ndiyo ambayo yako juu ama Serikali ndiyo iko juu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna mashaka na utaratibu mzima, lakini kama alivyosema kaka yangu, Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Mbatia kwamba, tatizo hapa lilianza kwa Serikali yenye. Serikali ilipoanza kubishana yenye kwa yenye makampuni *yaka-take ile advantage*. Tangu lini makampuni haya ya simu yakawapenda Wananchi wakati tunajua uwekezaji wao ni kwa ajili ya kupata faida tu? Leo wanasema katika ile bilioni 170 na kitu wao watachangia bilioni 30; wanazipataje? Kwa nini ushindwe kuchangia shilingi 1,000 useme utachangia bilioni 30? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna mashaka, Muswada ni mzuri hatuna tatizo nao kwa sababu lengo leke ni zuri, kwa ajili ya kwenda kuwasaidia Wananchi wetu.

Lingine limesemwa katika taarifa kwamba, Muswada huu utawaondolea adha Wananchi. Mimi nafikiri kilichofanyika hapa ni ile funika kombe mwanaharamu apite. Leo umeondoa shilingi 1,000 katika Serikali lakini unaenda unaongeza kwenye kodi kutoka asilimia 14.5 kwenda asilimia 17; hivi unafikiri makampuni ndiyo yatakayolipa ni Wananchi hawahawa; sasa mnawapunguzia kitu gani? (*Makofii*)

Ninafikiri hapa kuna haja ya kupata malezo vizuri zaidi; bado Serikali ituambie ni kwa nini wameshindwa kukusanya kodi hii kuanzia mwezi Juni tulipoipitisha hapa Bungeni? Bado Serikali hajatoa sababu zenye mashiko, kwa katuambia tu kwamba hali haiwezekani; sasa hii ni Serikali ama ni Sirikali? Kitu hiki hakiingii akilini, hebu tupeni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED]

maelezo, Bunge lilipitisha mwezi Juni hii Sheria, leo Desemba mnasema mnaileta haraka kwa Hati ya Dharura ili Januari muanze kukusanya na wale mliowakosesha maji na umeme kule mpaka makampuni yamekwenda Mahakamani ndiyo mmeanza kushituka kwa sababu mnawaogopa! Haya mambo hayaeleweki.

Mheshimiwa Spika, nirudie hapa hapo kwamba, hii itasaidia kuondoa adha vilevile kwa Wananchi katika hii kodi ya shilingi 1,000. Lazima tuangalie mbele na nyuma, sijui kama Serikali imefanya tathmini, unaposema unaongeza ushuru katika huduma nyingine za Mawasiliano, *Fax*, *Internet*; unajua sasa hivi wanafunzi wetu wengi wanatumia mitandao ya *internet* kujifunza. Sasa leo unakwenda kuwawekea tena ushuru wa ziada pale, hii sidhani kama Serikali imefanya tathmini ya kina kujua utawaathiri kiasi gani hawa wanafunzi ambao wanatumia mitandao hii kwa ajilli ya kujipatia elimu?

Umesema utaongeza katika *fax*, sasa tunapata mashaka na mlolongo mzima wa ubadilishaji wa Sheria hii. Hii Sheria ilikuwa iwe rahisi sana kuitekeleza kama Serikali ingalikuwa inasikiliza maoni ya Wabunge. Tulisema hapa ule mtambo wa *TCRA* ufungwe haraka, haya yote yasingalijitokeza na Serikali ingalikuwa tayari imeshapata mapato yake. Leo kutuambia makampuni yamekataa hata hivi yatachangia billioni 30, ni kitu ambacho kinatupa mashaka makubwa! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nirudi niseme kwamba, simu hizi zinatumika Tanzania nzima kwa maana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa hapa kilichozungumzwa ni maji na umeme vijjini, lakini na kule kwangu Kiuyu, Mjini Kiuyu, Kangagani na Changamdo, wanatumia hizi simu. Sasa tunataka kujua katika hizi bilioni 178 ambazo zimekusudiwa kupelekwa katika vijiji kwa ajili ya umeme na maji; kwa upande wa Zanzibar watafaidikaje na fedha hizi?

Tunaomba tupate maelezo, kwa sababu watumiaji wa mitandao hii ya simu, *internet fax* ni Watanzania wote

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED]

pamoja na wale walioko Visiwani. Sasa ni vyema ukatuweka wazi ili tujue upande wa pili wa Muungano watafaidikaje na fedha hizi. Je, watapelekewa kwa ajili ya maji vijijiini kwao ama watapelekewa kwa ajili ya umeme katika vijiji vyao? (*Makofî*)

Tunaomba hili mliweke wazi na nitaunga mkono hoja hii pale tu Waziri atakapoturidhisha katika hili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina!

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii na mimi nichangie kwa kifupi, kwa sababu ni kitu ambacho kwetu sisi na Watanzania kwa ujumla, kina faida kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, siyo vizuri sana kugombea fito wakati mnajenga nyumba moja. Muswada ulioko mbele yetu ni vizuri tuupitishe bila kuchelewa kwa sababu tumechelewa sana.

Kila Mbunge hapa kwenye eneo lake, kwenye Jimbo lake, anahitaji maji na umeme. Hata kule Njombe kwako Mheshimiwa Spika, unahitaji umeme na maji. Sasa pesa hizi shilingi bilioni 178 ambazo zilitengwa zikafanye kazi ya kuleta miundombinu ya maji na umeme ni vizuri sasa tusichelewe ndugu zangu, tusileté maneno mengi, tunahitaji pesa hizi zikafanye kazi kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi wetu. Ninawashauri sana Waheshimiwa Wabunge, tusichelewe hata kidogo tumeshachelewa. (*Makofî*)

La msingi, naiomba Serikali, hizi shilingi bilioni 30 ambazo makampuni ya simu yameahidi kuzitoa, zitoke haraka iwezekanavyo kwa sababu wameahidi wao wenyewe kwamba watazitoa, zichelewe vinginevyo itakuwa ni tatizo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

Mheshimwa Spika, nilishauri wakati nachangia kwenye utekelezaji wa Taarifa ya Mheshimiwa Chenge kwamba, suala la *simu card* limeleta matatizo sana. Vilevile wenzenetu Wizara ya Fedha wakaangalie upya ule utaratibu wa *transfer money*, maana nao una matatizo. Kwa kufanya hivyo, tunaweza tukawa tunapitisha mambo hapa tunakosa mapato kwa sababu kule juu kuna vizingiti.

Naomba kila tunaposhauri hapa na kazi yetu ni kuishauri Serikali, tunapoishauri Serikali basi nayo ikafanye kazi ambayo tumekusudia.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani, kwa siku ya leo tusipindishe maneno, tunataka tupate umeme na maji. Tuharakishe tupitishe *Bill* hii ili Serikali ikafanye kazi yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Silinde.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Hali ya mapato yetu ya ndani si shwari, Taifa linapungukiwa na fedha nyingi sana kulingana na mahitaji ya Taifa na sisi tunaendelea kuwa tegemezi. Taifa linaendelea kuwa tegemezi na linaendelea kuwa na deni kubwa sana. *We are highly indebted* na hatuna namna ya kutoka hapo zaidi ya kujimarisha sisi kimapato tuweze kujitegemea kimapato.

Mheshimwa Spika, kwanza, niseme kwamba, nilikuwa mionganini mwa Wajumbe ambao ultuteua kuwa kwenye Kamati ya kuishauri Serikali kuhusu mapato. Naendelea kukushukuru wewe kwa kunipa usoefu huo. Wenzetu Kenya mpaka hivi sasa kibajeti wanajitegemea kwa asilimia 98 kwa fedha za ndani, sisi bado tuko kwenye asilimia 60 ya kujitegemea kwa mapato ya fedha zetu za

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

ndani, asilimia 40 huku kushuka ambayo inabadilika kila mwaka ndiyo hasa tunajitegemea kwa fedha zetu za ndani.

Mheshimwa Spika, hapa si pazuri sana, lazima tutoke. Kama wenzangu walivyozungumza, lazima Watanzania wakubali kulipa kodi. Ukitaka maendeleo lazima ukubali kulipa kodi. Hakuna muujiza ambao tunaweza tukaufanya tukawaambia Wananchi tutawaleta barabara, tatawaleta umeme, halafu wasilipe kodi. Nazungumza maneno haya na Wananchi wangu wa Kisese wanansikia, ni lazima Watanzania wote tukubali kulipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutegemea fedha za watu huku kunatudhalilisha sana; kwanza, fedha haziletwi kwa wakati. Mambo tuliyowaahidi Watanzania mengine ya toka mwaka 2005 mpaka leo tumeshindwa kuyatekeleza kwa sababu ya kukosa pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata mimi pia nilishangaa sana, huo utaratibu uliotumiwa na malalamiko yaliyotolewa baada ya kupendekeza kodi hii na baadaye tukaipitisha kama kodi rasmi. Utaratibu wa kodi unajulikana kwamba, kila inapofika nusu mwaka mnafanya *mid-year review*, mnaona yanayowezekana na mnakuwa na ushahidi wa kitakwimu ya kwamba, hii kodi inawezekana na hii haiwezekani. Kodi hii imepingwa hata kabla haijaanza kutumika na kabla hatujaanza kuona yale madhara yake. Tungeona kitakwimu baada ya miezi sita, kodi hii ikawa imepingwa hata kabla haijafanya kazi. Niseme kuwa, tuna Kamati ya Bajeti sasa hivi tuwe na ile Taarifa ya *Mid-Year Review* ambapo tutaangalia kodi zetu tulizozipendekeza zinafakiwa au hazifanikiwi na kama hazifanikiwi tufanye nini. Tunaruhusiwa kufanya mabadiliko katika *mid-year review*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sekta hii ni muhimu sana, lakini inachangia katika mapato yetu ya ndani mpaka sasa hivi kwa asilimia 5.2 tu licha ya ukubwa wa Sekta yote. Tukijilinganisha na mapato ya wenzetu wanayopata, kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

mfano, katika *Corporate Tax*. Mwaka 2010 takwimu zilionesha Tanzania iliweza kukusanya *1.7 million U.S. Dollar* katika kodi ya mapato wakati wenzetu Kenya walikusanya *79.3 million US Dollar*, Uganda *31.3 million* na Rwanda nchi ndogo *14 million*.

Sasa unaona jinsi ambavyo sisi hata hayo makampuni ambayo leo yanalamika kutokutendewa haki, licha ya sisi hata kwenye *market* tuna wateja wengi, maana *population* tuliyonayo, maana simu hapa nchini zina wateja wengi wa mtaji huo wa watu milioni 44, lakini bado mchango wake katika kodi ndio huo kwa maana tu ya kodi ya mapato ukilinganisha ukaona jinsi ambavyo sisi tuko chini sana. Utafiti unaonesha kwamba, kila mwaka kwa simu tu tunapoteza bilioni 600, kodi ambayo ilikuwa halali kabisa kuchangiwa.

Mheshimiwa Spika, tumezungumza mambo mengi sana na kama unaweza ukazipata leo bilioni 600 kwa kufanya marekebisho tu ya Sheria zetu, ukaongeza usimamizi katika maeneo ya simu ambayo hayajasimamiwa sawa sawa, kwanza, gharama za uwekezaji, wawekezaji wetu kwa maana ya ununuzi wa mashine, kwa maana ya ununuzi wa mitambo na kwa maana ya teknolojia wanayoileta, hakuna *control* yoyote iliyopo. Katika Sheria zetu hatujaweka kifungu chochote cha sheria cha kuwa-*bind* wala cha kufuatilia kujua wanakokotoaje kuifikia gharama halisi.

Wanatumia gharama kubwa sana ya mapato yao mpaka asilimia tisa ya mapato yao katika *management and service fee*. Ukizingatia kwamba makampuni yote haya ya simu ni makampuni tanzu ya makampuni mama. Kwa hiyo, ukiangalia pale kwenye *management fee* yapo makampuni mengine yanatumia asilimia sita ya mapato yao yote, ambapo sisi tunaweza tuka-*cap* kwenye sheria zetu tukasema sasa badala ya *management fee* kuwaachia makampuni yajipangie yenye na ukizingatia kwamba haya ni makampuni tanzu, tuweke *cap* tuseme basi *management fee* kuanzia sasa itakuwa asilimia mbili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

Sasa hivi utakuta mwingine asilimia sita, mwingine asilimia nane na mwingine mpaka asilimia kumi, hiyo yote ni *management fee*.

Ukija kwenye loyalty nako hakuna *control* wala sheria yetu yoyote ile haijaweka *control* ya *loyalty*, wanalipa wanavyoweza wao na ukizingatia hivyo hivyo kwamba haya ni makampuni tanzu, kwa hiyo, wana *trade off* kwa kadiri wanavyoweza na makampuni yao mama. Ukiingia kwenye *promotion* nako vilevile makampuni sasa hivi yanatumia mpaka asilimia tisa mpaka kumi ya mapato yao yote wanasema hii ni *promotion*, wanasema shabaha yao kubwa ni kupunguza kodi, shabaha yao kubwa ni kupunguza *liability, tax liability* mwisho wa siku.

Mheshimiwa Spika, ninasema na hapa ninaendelea kusema kila siku kwamba, kuna suala linalotusumbua sana katika makampuni mama pamoja na makampuni tanzu; nalo ni Sheria yetu ya *Transfer Pricing*. Sheria yetu ya Mapato ya Mwaka 2004 (*The Income Tax Act of 2004*), Kifungu cha 33 (1) na (2) kimeizungumzia *tax*, kimeizungumzia *transfer pricing*, lakini *guidelines* na *regulations* za namna gani sasa unaweza kukokotoa na kufikia bei halisi, hatuna Kanuni hizo katika Sheria yetu hiyo ya Mapato. Wenzetu wa *TRA* wamefanya jitihada za kuhakikisha Kanuni hizo zinapatikana, walishaziandaa Kanuni, walishaandaa *guidelines* na zipo mezani kwa Waziri wa Fedha, leo ni zaidi ya miezi minane!

Kwa nini mapato kama haya tunayaacha yapotee? Nimesema bilioni 600 zinapotea katika eneo hili na hao watu wenye makampuni ya simu hawana hata aibu hata kuja na malalamiko kama haya wakati Taifa hili wanaliibia kwa kiwango kikubwa mno na ushahidi wa kitakwimu upo ambaa unaonesha dhahiri kwamba, fedha nyingi zinapotea.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Kenya hii Sheria ya *Transfer Pricing*, hizi *guidelines* na *regulations* za *transfer pricing* kwa kujua matatizo sasa hivi ya *multinational*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

companies, Sheria hizi zipo toka mwaka 2006 na wenzetu Uganda zipo, tumebaki sisi tu; tatizo ni nini kuzitangaza hizi Sheria kwenye Gazeti la Serikali ili zianze kufanya kaz?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini Kanuni hizi zitatangazwa kwenye Gazeti la Serikali ili zianze kutumika? Kabla hatujaingia kwenye bajeti ya mwaka unaokuja, tuelezwe namna Serikali ilivyojipanga kupambana na ghamama za uwekezaji ambazo zinafanya makampuni ya uwekezaji, *management and service fee, loyalty, promotion* na mambo mengine, ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata haki yao ya kodi kutohana na makampuni ya simu.

Tumeelezwa kwamba, huu Mtandao wa *Telecommunication Traffic Monitoring* tayari ulishawekwa, basi tuelezwe toka uwekwe tunaweza tukalinganisha kwamba tumeanza kupata mafanikio sasa au hapana?

Mheshimiwa Spika, niliongea hata kwenye Bunge lililopita kwamba, Serikali lazima tupunguze matumizi yetu kwa namna yoyote ili tubaki na fedha nyngi sana kwa ajili ya kumaliza matatizo ya Watanzania. Baada ya Bunge hili kulalamikia matumizi ya Serikali, Serikali ilikubali kwa maandishi na kila kifungu Waziri wa Fedha aliandika kwa maandishi kwamba, tumekubali kupunguza matumizi ya fedha za Serikali kwa fedha kadhaa. Ukipunguza zile barua za Waziri wa Fedha zinifikia bilioni 283, ambazo alisema hizi tunaweza tukazipunguza kutoka kwenye matumizi yetu ya kawaida na bado hakutaathiri utendaji wa Serikali.

Cha kushangaza, bajeti ilipoletwa, zilipendekezwa tu baadhi ya kodi kuongezwa viwango pamoja na kodi mpya, hili suala la kupunguza matumizi ya Serikali halikutajwa. Waziri wa Fedha wakati ana-*wind up* akasisitiza akasema, Serikali imekubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mpina.

Waziri wa Fedha aliogopa siku ile nitakataa Bajeti

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

ya Serikali akasema, nimekubali ushauri wa Mheshimiwa Mpina, tutapunguza matumizi ya Serikali. Itakapofika kwenye *mid-year review* tutaleta Bungeni mchanganuo wa fedha tulizozipunguza kwenye matumizi ya kawaida. Nikasikiliza mpaka mwisho, bilioni 283 walau basi ambazo waliji-*commit* kwa maandishi, zingeletwa hapa ambapo leo ndiyo tunazungumzia miezi sita ya bajeti imepita, lingeletwa lile jedwali, matumizi yale yamepunguzwa ya bilioni 283 na kupelekwa kwenye Miradi ya Maendeleo ambayo itakuwa imependelezwa na Serikali na sisi tukatoa kibali.

Mheshimiwa Spika, hili halijafanyika hapa Bungeni na hatuwezi kukubali. Tuliahidiwa kwa maandishi, tunayo maandishi, kama haitawezekana, basi tutaleta Muswada Binafsi kwa ajili ya kuhakikisha haki hiyo imetendeka kwa sababu haikuwa mzaha. Ilikuwa ni *commitment* ya Serikali kupunguza matumizi yake ya kawaida. Matumizi haya ya kawaida, ninajua yalivyokuwa, katika mapendekezo ya bajeti, bajeti zetu kila mwaka huwa kuna utaratibu wa kusema kwamba, kila Wizara ongeza asilimia tano ya mwaka jana. Kwa hiyo, watu wameanza hivyo toka mwaka 2000, ongeza asilimia tano, ongeza asilimia tano, hadi leo tuna mzigo mkubwa wa matumizi ya Serikali kuliko hata mapato yetu ya ndani.

Tulipofikia hapa, kama unaweza ukatumia fedha kuliko mapato yako ya ndani kwa matumizi ya kawaida, huwezi ukatoka kwenye ile *web* ya utegemezi na kama huwezi kutoka, nchi hii itapigwa mnada siku moja. Kama unaweza kutumia kuliko rasilimali zako, mwisho wa siku aliyekukopesha atasema basi naomba rasilimali zako zote nirejeshe fedha yangu ambayo nilikukopesha. Kwa hiyo, tusifike huko, tusiendelee kuwa wategemezi wakati tunaweza. Tukipunguza matumizi yetu ya kawaida, tutawekeza vyta kutosha katika miundombinu ya uchumi. Tutahakikisha Wananchi wetu wanapata maji, tutahakikisha Wananchi wetu wanapata umeme na tutahakikisha Wananchi wetu wanapata maendeleo ya haraka kama ambavyo tuliwaahidi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LUHAGA J. MPINA]

Mheshimiwa Spika, haya mambo yanawezekana, ni maamuzi tu, Serikali wakiamua na wakitusikiliza vizuri tunaweza kutoka hapa. Leo tunaenda kwenye bajeti mpya, niliomba zile sheria zote, nimesikia hatujaambiwa hapa Bungeni kwamba, kuna Bunge litapatikana mwezi wa kwanza. Naomba sana zile sheria zote zinazohusu Marekebisho ya Kodi, kabla hatujaingia kwenye Bunge la Bajeti, ziletwe muda ule ili tuweze kuwekana sawa. Tunapoenda kwenye Bajeti yetu tuwe na uhakika kwamba, Sheria zimefanyiwa marekebisho kikamilifu. Kama tulivyosema, Sheria ya VAT ya Mwaka 1967 irekebishwe ili kuondoa misamaha isiyokuwa na tija, Sheria ya TIC pamoja na Sheria zingine ambazo tunaweza kuzirekebisha, tutakapoingia kwenye Bajeti tusivutane tena. Sasa na hayo yote niliyoyazungumza haya ya *transfer pricing*, mwezi wa kwanza lazima tuhakikishiwe na Serikali kwamba, imekaa sawasawa; kwa sababu nayo inahusu bajeti yetu tutakayoanza nayo. (*Makofii*)

Mheashimiwa Spika, uzalendo wetu tutauthibitisha kwa kutumikia, kwa kuweza kumudu na kutimiza majukumu yetu. Naishukuru Serikali kwamba, Sheria ya Manunuzi sasa wameshatangaza kama Waziri alivyosema, wametangaza kanuni na sasa hivi Sheria hiyo inatumika. Sheria ile itatusaidia sana, kwa mfano, tutakapowapata wale watu walitorosha fedha nje ya nchi, Sheria yetu tumeiweka vizuri sana katika Kifungu cha (104), ambapo watu hao tutawafilisi kwa ajili ya kuhakikisha fedha zile zimerejeshwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sana hii hoja ambayo imetolewa hapa mbele yetu. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Shekifu.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii na mimi nichangie Muswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza kabisa,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

naipongeza Serikali kwa kusikiliza kilio cha Wananchi. Pamoja na kuwapongeza kwa kusikiliza kilio cha Wananchi na kutoa hii tozo ambayo Wananchi wengi walipingga, lazima tuwaambie kwamba, hebu jaribuni kuacha ile kitu inaitwa ujeuri. Kwa sababu hili suala tuliwashauri mwanzoni na kama tuliwashauri mwanzoni, tungekaa pamoja tukaelewana, maana yake leo tusingerudi tena hapa hapa Bungeni kuja kujadili jambo lile lile. Matokeo yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, nimewapongeza Serikali kwa kutoa hii tozo ya shilingi 1,000 kwa Wananchi. Jambo la pili, nawapa ushauri kwamba, mambo kama haya katika Bunge lililopita la Bajeti tulipigana kweli ndani ya Bunge kupinga huu Muswada, lakini hatukuelewaka. Hii yote tunasema ndiyo ujeuri. Huu ujeuri ungeachwa, maana yake leo hii miezi sita iliyopita tungekuwa tumekwishakusanya kodi na tungefika tunakokwenda. Mambo haya yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara, hata jana, ninyi wenyewe mlisihuhudia, Mawaziri hawa tuliwaambia jamani watu wanakufa huko wakapuuzia, matokeo yake jana wote wameondoka nje. Sasa utaratibu huu ndiyo umeliponza hili Taifa.

Mheshimiwa Spika, malengo ya ongezeko la kodi ya ushuru siyo mabaya ni mazuri kabisa. Lengo lake tunataka tupate fedha kwa ajili ya maji na tunataka tupate fedha kwa ajili ya umeme vijiji. Sasa tupeni uhakika wa ukusanyaji wa hizo fedha; uhakika upo? Zisije zikawa stori zile zile, tunatoka hapo, kesho tunaambiwa kuna *court injunction*, miezi sita inapita, tunarudi tena katika Bunge, hatutawaelewa. Msiwe ni watu wa stori ambazo hazitekelezeki. Kwa hiyo, haya nayo lazima mtuhakikishie kwamba, tumekaa tumejadili na wadau wote na wadau wamesema tuna uhakikisha hii kodi tunayokwenda kuipitisha hakuna jambo lolote baya litakalotokea baada ya hapo.

Mheshimiwa Spika, nizungumze tu kwamba, kuna baadhi ya mambo ambayo tunahitaji ufanuzi katika hili ongezeko la kodi. Ongezeko la sasa tunatoka katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

asilimia 14 mpaka asilimia 17. Je, halitaathiri ongezeko la watumiaji wa simu, yaani zile gharama kwa sababu tumeondoa elfu moja, tumekwenda kufanya *replacement* kutoka asilimia 14.5 mpaka asilimia 17 ya ushuru wa bidhaa iliyoko sasa? Sasa tujue, anayelipa hapa ni nani ni mtumiaji wa kawaida Mwananchi ama ni makampuni ya simu kwa sababu naona tume-change strategy kutoka kwenye shilingi elfu moja kwenda katika asilimia 2.5?

Jambo lingine, Waziri wa Fedha pamoja na wengine mtakapokuwa mnajibu mtueleze, kwa sababu takwimu za sasa zinasema *subscriber* kwa kwa maana ya watumiaji wa *line* za simu mpaka sasa hivi ni milioni 28. Sasa isije ikawa ongezeko hili la asilimia 2.5 kesho tukaambiwa *subscriber* wa simu wako milioni 14, kwamba, kutoka milioni 28 mpaka sasa hivi milioni 14. Serikali itueleze hao *subscriber* ambao wapo sasa hivi tutapata kiwango gani, tusiwe tu tunasema kutokana na hii kodi kwa makadirio tutapata bilioni 148 na hivi, tuelezwe *in figures*, hapo ndiyo tutakuwa tunaelewana.

Jambo la tatu ni kwamba, Sheria ambayo tunaipitisha sasa hivi imesema itaipatia Serikali bilioni 148. Tunataka ufanuzi Wananchi waelewe; hizo bilioni 30 ambazo zinakwenda kuongezeka katika kile kiwango cha bilioni 178 ambazo tumezipanga, makampuni hayo yanayolipa yatatoa kama msaada, hisani, rushwa ama ni kitu gani? Wananchi waelezwe hilo ili tuweze kupatiwa ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, lakini mambo mengine ambayo tumekuwa tukiyazoea kila siku, jamani Serikali mtueleze ni kwa nini mnashindwa kukusanya kodi? Tusipolezana ukweli kwa nini tunashindwa kukusanya kodi, maana yake hapa kila siku zitakuwa ni stori zile zile. Tunataka tujue kama hamuaminiki ama siyo wabunifu maana kuna mambo mawili; moja, inawezekana huaminiki; na pili, inawezekana siyo mbunifu wa vyanzo bora kabisa nya kodi. Hili nalisema kwa sababu Wananchi wenyewe hawalipi kodi. Kwa nini? Kwa sababu hawana imani na sisi Viongozi na Serikali ndiyo maana watu wanakwepa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

Leo nakwenda dukani, kwa mfano, unanunua tairi la gari, unaambiwa kwa risiti shilingi laki nne na ishirini, bila risiti shilingi laki tatu. Kwa akili ya kawaida tu tuongee ukweli, kwa Mtanzania wa kawaida tu, *difference* ya shilingi lami moja na ishirini kweli unaweza ukailipia Serikali? Tuongee tu katika hali ya kawaida, unaona Serikali kwa staili hii itaendelea kuwa inakosa mapato kwa kiwango hiki. Lingine inawezekana hata watu waliopo, unajua hata kwenye harambee huwa watu wanaangalia, wanasema hii harambee ukimwita Silinde tunaweza tukapata shilingi milioni moja, lakini ukimwita Mheshimiwa Makinda tutapata shilingi elfu hamsini. Kwa hiyo, wanaamua kumchukua Silinde, wanamwacha Makinda. Sijui kama mmenielewa? Sasa inawezekana hata kwenye hii Serikali hali ikawa hiyo. Sawa jamani? Kwa hiyo, lazima tuambiane katika hilo. Inawezekana hamuaminiki au mmekosa ubunifu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mambo mengine machache kama matatu hivi ambayo kila siku Bunge lako Tukufu limekuwa likiyasemea. Ripoti ya Shirika la Fedha Duniani (*IMF*) ya Mwaka 2011, ilijaaribu kuainisha watu wanaopaswa kulipa kodi nchini kwetu. Kwa Tanzania walitoa takwimu za watu milioni 15 wanaopaswa kulipa kodi. Leo hii katika nchi yetu hiyo hiyo, watu wanaolipa kodi ni milioni 2.5 tu. Sasa unaweza kuona kuna *difference* ya watu milioni 12.5. Wakati hapo hapo katika nchi ya Kenya, takwimu hizo hizo, watu wa *IMF* walisema watu wa Kenya wanaopaswa kulipa kodi ni milioni 12.5 na wanaolipa kodi ni watu milioni 9.5. Sasa hapa hatuoni kama kuna shida kwenye ukusanyaji wa kodi katika Serikali yetu?

Mimi naamini angalau kutoka hao waliopaswa kulipa ambaa ni milioni 15 tungefikia watu milioni tano tu, maana yake hata leo tusingekuja na hili ongezeko la sheria kutoka asilimia 14.5 hadi asilimia 17 kwa sababu tungekuwa na uwezo wa *ku-cover deficit* ambayo ilikuwepo.

Jambo lingine ni misamaha ya kodi. Tumekuwa tukisema kila siku kwamba, Taifa letu lisamehe kodi kwa kiwango cha asilimia 4.5 ya Pato la Taifa. Tumelalamika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

sana kila siku na lazima Wananchi wafahamu, Pato la Taifa letu kwa sasa hapa tulipo linafikia dola bilioni 28. Sasa angalia, katika nchi zote katika Afrika ya Mashariki, watu wanaolipa kodi, yaani misamaha ya kodi katika nchi zote Afrika ya Mashariki ni chini ya asilimia mbili. Sisi Tanzania peke yetu tuko asilimia 4.5.

Sasa niwaambie kitu kimoja, hii tofauti ya asilimia 2.5 tungekuwa tunakwenda katika ile asilimia ya nchi zetu za Afrika Mashariki, Serikali ilikuwa na uwezo wa kupata dola milioni 700, karibu trillioni moja. Tungekuwa tuna-cover bajeti za Wizara ngapi? Hapa leo tunajadili bilioni 178, lakini kupunguza tu ule msamaha wa kodi kutoka asilimia 4.5 mpaka asilimia mbili, tulikuwa na uwezo wa kupata dola milioni 700. Kwa hiyo, lazima tuwe tunaangalia, muda mwagine tunaanzisha vyanzo na wakati vyanzo vyenye uhakika viro na tunakwenda kwenye vyanzo ambavyo vinawaletea machungu Wananchi wetu.

Jambo la mwisho ambalo nataka nilisemee ni uamuzi wa kununua mtambo kwa ajili ya kufuatilia masuala ya simu. Bunge lako Tukufu mwaka 2007 lilipitisha uamuzi huo, lakini leo miaka saba, wakati huo watu wa Rwanda waliamua ndani ya mwaka mmoja wakawa wamenunua mtambo wa kurekodi simu. Sasa tujiulize, tumekosa kiasi gani cha fedha kwa miaka saba kwa kushindwa kuchukua uamuzi?

Sasa haya ndiyo makosa mengi ambayo tumekuwa tukiyafanya na tumekuwa tukishindwa kujadili mambo ya msingi kama haya. Hatuwezi kuendelea kujadili kodi ambazo zinakwenda kuwagusa Wananchi moja kwa moja, wakati kuna kodi za msingi na za uhakika ambazo hazina wasiwasi wowote, Serikali inashindwa kuzichukua. Ndiyo maana hapa tunasema kunakuwa na wasiwasi, huwezi kumwambia Mwananchi Mzalendo kama wewe mwenyewe Mbunge siyo Mzalendo. Mbunge unalalamikiwa kwa kuchukua posho, Mbunge unalalamikwa kwa ujangili, Mbunge unalalamikiwa kwa ula rushwa halafu unakwenda kumwambia Mwananchi awe Mzalendo; *how?*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

Mwalimu analala kwenye nyumba haina hata cement halafu unamwambia awe Mzalendo. Anakuwaje Mzalendo wakati mtoto wako Mbunge anasoma *International School?* Ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, tuushawishi uzalendo kwa vitendo na vitendo vyenyewe ni nini? Hizi kodi tunazozizungumza, zichukuliwe hatua. Punguzeni misamaha ya kodi. Uamuzi ambaao tumechukua sasa tunataka tujue Serikali itakuwa inapata kiasi gani kutoka kwa *subscriber* wake wa simu. Hii nilikuwa nikilisema kwa sababu kwa mfano mimi Mbunge nina *line* nne, sasa hii gharama ikipanda nita-stop *line* mbili, maana yake *subscriber* wawili wameshapungua, lakini ni mimi mmoja. Si ndiyo jamani? Kwa hiyo, hili naomba lieleweke. Tuzungumze uzalendo kwa vitendo, tusizungumze uzalendo kwa maneno. Tumekuwa Wazalendo kwa maneno zaidi.

Mheshimiwa Spika, ningeomba pamoja na kwamba ninaafiki hili suala kwa sababu tu ya mahitaji ya maji, lakini mahitaji ya maji miaka 50 jamani, bado ni mateso kule vijijini. Nitarudia tena, watu wanaopiga kura ni wengi. Serikali ya Chama cha Mapinduzi mmekuwa mkisema kila siku, wateja wetu wako vijijini, wapiga kura wetu wako vijijini, lakini mnawanyanya zaidi watu wa vijijini kuliko watu wa mijini. Waangalieni kabla ya mwaka 2015 wapate maji safi, wapate umeme, wapate barabara na wao ni binadamu na asilimia 80 ya Watanzania wanaishi kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Shekifu, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Muhongo.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe na pia naishukuru Kamati ya Bajeti kwa kuridhia na kutuletea ushauri wao, tukubali mabadiliko haya.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, yale ambayo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. HENRY D. SHEKIFUJ]

yanasemwa na yamesemwa na mzunguzaji aliyepita kwamba, tufanya juhudzi za kuwahudumia Wananchi hasa wale wa vijijini, ndyo haya tunayoyazungumza, wala si mageni. Tunachokiomba hapa, tuidhinishe kodi tupeleke maji na umeme vijijini; ndilo tunaloliomba. Sasa hitilafu ndogo ndogo ambazo zipo, ushauri lazima tuupokee. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mimi nina wasiwasi katika maeneo machache tu. Nianze kwa kusema, *collective responsibility* katika utekelezaji ni jambo muhimu sana. Tuiombe Serikali kwamba, kwa kweli tuwajibike kwa pamoja katika utendaji. Mimi nimemsikiliza sana Mheshimiwa Mbatia, kama tumekubaliana jambo basi kama lina makosa tuzungumze wote kama Serikali. Tusitofautiane kwa kutaka umaarufu au kwa njia yoyote ile, kundi la Chama au kundi la mtu binafsi. Ndiyo haya tunayosema, masilahi yanayohusu Taifa, wote tujikite pale tulioke Taifa letu. Hakuna asiyejua faida ya maji, hakuna asiyejua faida ya umeme vijijini. Pia ni kweli kwamba, tutakapopeleka umeme kwa ahadi tulizotoa, mabadiliko makubwa ya uchumi katika nchi yetu yatatokea na wote tunakubaliana, pande zote. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba katika hii tafrani iliyotokea, ambayo sikfurahishwa nayo, kwanza, niseme tu kwamba, watu hawa binafsi, wenyewe mashirika yao binafsi, tuwe waangalifu sana tunapo-deal nao kama Serikali. Tuwe wafanyabiashara kama wao. Mimi nimekulia katika biashara, uzee wangu wote huu ni kwenye biashara na Mfanyabiashara yejote atavutia upande wake. Hivi bilioni 30 wanazitoa wapi ili wafidie pengo kama hawapati faida? (Makof)

Mimi sitaki kuzungumza sana kwa sababu na mimi kama ningepewa nafasi hiyo kama Mfanyabiashara, haya mambo yapo, ndyo biashara. Sasa yule unayezungumza naye ndyo anapaswa kuwa mjanja katika kukuhoji na kukuzunguka. Tuliamua kodi ishikwe. Sasa huyu anayekuja anasema hii ni ngumu kushika, tutalaumiana wenyewe,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. HENRY D. SHEKIFU]

hatutapata manufaa kamili. Sasa mimi nishauri, kwa sababu tumeshaingia kwenye mtego; kwanza, wazo la kukopa hela kipindi hiki ili tutekeleze Miradi hii bila kuchelewa ni muhimu sana. Wabunge tuiagize Serikali tukatafute hizo hela ambazo tungezipata mpaka nusu mwaka huu, tulipe tuzipeleke Mawilayani, Mikoani; zikatengeneze shughuli za umeme na maji. Sasa mimi naamini tunapozungumza, Serikali inasikia na inaya-note tunayoyazungumza. (*Makof*)

Pili, naiomba sana Serikali iheshimu matamko yake. Kwa sasa nina wasiwasi kwamba, tumekwenda nusu mwaka, Kamati ya Bajeti sijaiona taarifa yake. Tumekwenda kwa *performance* ya asilimia ngapi? Wameshawasilisha asilimia ngapi? Fedha zilizokwenda Mikoani na Wilaya ni kiasi gani; ni asilimia ngapi ya Bajeti? Inategemea, tunafika nusu mwaka, kwa hiyo, naamini asilimia 50 itakuwa imekwenda na ninasikia hata robo hajifika. Utatembeaje nusu mwaka na robo, *then* useme utamaliza katika kipindi cha nusu mwaka kilichobaki? Siyo rahisi sana. Ninaomba, ili Wananchi watuone tuko *serious*, ni lazima tutekeleze yale tunayotamka. Naiomba Kamati ya Bajeti, tumeomba iundwe Kamati hii kwa kutusaidia Wabunge kufuatialia Serikali itekeleze yale yaliyoahidiwa, ndio tulioomba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tusaidie uwabane. Ninaamini kwa umoja wetu tulionao sasa katika Bunge, kama tulivyoonesha jana, sasa tunaonekana ni Bunge la kweli. Maana suala lenye masilahi kwa Taifa letu tutalisimamia kwa pamoja na hili ndio linalohitajika katika Bunge, tunaacha vyama vyetu tukiingia mlango ule. Tukiingia humu ni kitu kimoja, tusivitumie vipaza sauti hivi kwa kutafuta umaarufu wa mtu binafsi au kundi ili tukija hapa tuzungumze jambo moja la kuleta maendeleo yetu.

Ninaomba sana Serikali ikubaliane nami kwamba, udhaifu ambaou umeanza kujionesha na siyo kwamba umeanza upo, hasa mshikamano na kutekeleza wajibu. Sisi kama Wabunge, tunaahidi sasa tunashikamana na tutahakikisha maendeleo kwa Wananchi yanapatikana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. HENRY D. SHEKIFU]

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kulishukuru sana Bunge lako na kuliomba tuendelee kutetea haki za Wananchi wetu. Mimi naamini Muswada huu una lengo jema sana. Tuzitafute fedha hizi na bahati nzuri tumethibitishiwa kwamba, hazitaathiri makusanyo yaliyotegemewa. Kwa kuwa hazitaathiri makusanyo yaliyotegemewa, kwa maamuzi haya tunayofanya leo, basi fedha zipatikane kwa kukopa kwanza ili tulipe hayo madeni baadaye na maendeleo vijiji yapatikane.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Muhongo!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuungana na Wabunge wenzangu kwamba, Muswada ulioletwa ni muhimu sana na nina imani wote tutakubali upite.

Kuna mambo ambayo sasa Watanzania lazima tuelezane ukweli na kama tunataka kweli kuwasaidia maskini na wanyonge wa Taifa hili ni lazima tufanye mageuzi makubwa sana ya kiuchumi. Bajeti yetu ya mwaka huu ni trilioni 18.24, makusanyo yetu ya TRA kwa mwezi hayavuki bilioni 800. Nikifuata wasemaji wa awali na hasa Mheshimiwa Mpina na wengine na Mheshimiwa Mbatia kwamba, inabidi tujitegemee kama nchi zingine wamesema Kenya wamefikia karibu asilimia 90; ni kwamba, ikiwa bajeti yetu ni trilioni 18.24, inamaanisha kwamba makusanyo ya mwezi yanapaswa yasiwe chini ya trilioni 1.52. Ukitaka kuwa na *balance* useme tulipaswa kuwa na makusanyo ya trilioni mbili kwa mwezi, lakini makusanyo yetu ni nusu ya hiyo, inamaanisha hatulipi kodi. Kweli Wabunge mna haki ya kueleza sisi Serikali tujitahidi kukusanya kodi, vilevile ni upande wenu Wabunge na Wananchi kwa ujumla lazima tuanze kulipa kodi. (*Makofi*)

Tuachane na kushabikia Mtanzania anakupatia chai na maandazi huku hakulipa kodi unamwona ni mtu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

mahiri. Hiyo tuachane nayo sasa. Mtu yeote anayekupatia zawadi na vinywaji na *entertainment* yoyote, jiulize kama amelipa kodi. Ninapenda Kamati ya Bajeti isifanye kazi na Wizara ya Fedha peke yake ni lazima ishuke kwenye Sekta ambazo zinapaswa kukusanya kodi ikiwemo na Sekta yangu ya Madini. (*Makofi*)

Ndugu zangu nilitoa takwimu hapa, Mererani kuna *Tanzanite*, tuna leseni 597, wanaolipa kodi hawavuki watu kumi na kwa miaka mitano watu wamelipa milioni 30. Miaka mitano inayofuata mingine ...

MHE. SPIKA: Umesema bilioni 30 au milioni 30?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Milioni 30. Nina takwimu hapa, ndiyo maana juzi nilitaka waniongezee muda niwapatie hayo. (*Kicheko*)

Watu ambao wanapenda ubaguzi, nikachukua wachimbaji maarufu 13 wa Kitanzania. Kwa miaka mitano wanaolipa kodi ni watano na hawavuki milioni kumi. Kwa hiyo, ni masikitiko makubwa. Ndugu zangu hilo ni la kwanza, kwamba, ni lazima sisi Watanzania wote mambo ya kushabikia mtu au kampuni, tuachane nayo na mambo ya kufikiria kwamba wanaokwepa kodi ni wageni tu tuachane nayo. Wageni na Watanzania lazima wote tulipe kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye Sekta yangu. Ndugu zangu huu Muswada ni muhimu kwa sababu Sekta ya Nishati inakua kwa kasi kubwa. Toka mwaka 1964, *TANESCO* inaanizisha, hajjawahi kufungia wateja 50,000 kwa mwaka. Mwaka jana ndiyo walipiga vigelegele wakafungua na *champagne* walivyouniganisha wateja 89,000. Mwaka huu wameshaunganisha wateja 138,000 na ndiyo maana nikasema mambo ya nguzo muwe na uvumilivu tutavileta hivi vifaa kwa sababu waombaji wamekuwa wengi.

Tuone umuhimu wa hii Muswada, ni kwamba, hizi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

fedha zinahitajika, kwa sababu bajeti ya REA kwa miaka miwili ni bilioni 881. Kwa hiyo, inamaanisha zaidi ya bilioni 400 kila mwaka. Haya mahesabu yamekuja, ukichukua Watanzania wanaotumia umeme kwa ujumla ni karibu asilimia 21, lakini ndiyo maana nimesema sikilizeni kwa makini salamu za Mheshimiwa Rais, atakuja na takwimu ambazo zinaonesha kasi ya kuweka umeme nchini mwetu, tumevuka hapo. Wakati mnaziangalia hizo takwimu kuna namna mbili ya kuziangalia.

Takwimu ya kwanza ni kusema wale waliounganishiwa (*connectivity*), ndiyo tunasema asilimia 21, lakini kuna wale wenye *access*, yaani kuna fursa, umeme umefika kijiji, huyo mtu ana fursa ya kupata umeme. Kwa hiyo, tunatengeneza takwimu zote mbili, hii ya *connectivity* tutaitoa mwisho wa mwaka, lakini hiyo ya *accessibility* tutaitoa mwezi Machi. Nina hakika itakapotoka mwezi Machi, mtaona tuko zaidi ya asilimia 30, tunakaribia asilimia 40 ya *accessibility*. (*Makofii*)

Hatuendi hivyo tu, tunapiga hesabu ya idadi ya wingi wa umeme ambao kila mtu anautumia. Mwaka 1011, ile *power per capital*, yaani ukichukua uwezo wetu wote wa kuzalisha umeme tukagawana na idadi ya Wananchi nchini mwetu, tulikuwa tuna *units 73 kilowatt hour. Units 73* inamaanisha kwa mwaka, sijui kwa nini maana *per capital* huwa ni kwa mwaka. Kwa hiyo, 73, mwaka huu tumeshafika 97, lakini malengo yetu ifikapo 2015 tuwe na *units 238* kwa mwaka.

Sasa linganisha hiyo na South Africa ambao wao wapo kwenye *units* zaidi ya 5000. Ndiyo maana sisi ni maskini na vijana wetu wanaenda South Africa kwa ajili ya kutafuta umeme tu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ninaomba huu Muswada upite, lakini unapoangalia suala la umeme lazima uwe na picha kubwa ya Afrika na ya Dunia nzima.

Tusikae tunajilaumu sisi wenyewe kwamba tuko nyuma, ukiangalia picha ya dunia inaonesha toka mwaka 2001 mpaka 2030, dunia nzima inahitaji karibu Dola za

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

Marekani trillioni 16 kwa ajili ya mambo ya umeme, ambayo ni matumizi karibu ya bilioni 550 kwa mwaka. Afrika ukitaka kuipatia umeme kufika mwaka 2030, unahitaji kutumia bilioni 300 na sisi tuko humu na ni heshima kubwa kwamba, Tanzania imechaguliwa kufanya *lobbying* ya kuweka nishati kwenye Malengo ya Milenia yanayotekelawa hivi sasa. (*Makofii*)

Sasa wapi tupate fedha? Kwanza, tulipe kodi na tusiwashabikie wasiolipa kodi. Pili, lazima tuongeze mbinu zetu za kukopa fedha. Mtu yejote ambaye yuko kwenye sayari hii hawezi kukimbia kukopa, kukopa ndiyo biashara. *GDP* ya Marekani mwaka huu ni karibu trillioni 15.97 na wao wameshakopa kuzidi hapo. Sasa kama Wamarekani ambao ni *the biggest economy on this planet* imevusha kwa nini sisi wadogo? Tunachopaswa kufanya, sehemu ambazo tunapaswa kukopa tukwepe ile mikopo ya kibiashara kwa sababu riba yake ni kubwa. (*Makofii*)

Mahali ambapo tunaweza kwenda kukopa sisi, mahali kama fedha za *World Bank* zinachukua muda lakini riba yao huwa ni ndogo, ni 0.2 halafu wanawapatia kipindi cha mpito hamlipi chochote kwa miaka mitano, kumi na deni mnakuja kulimalizia baada ya miaka ishirini au thelathini. Hiyo ni njia nyepesi ya kupata fedha nydingi za kutengenezea Miradi. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tumeshaanza kufanya *lobbying African Development Bank*, maana *ceiling* yake inasema kwa miaka mitatu tusivuke mkopo wa dola milioni 600. Kwa hiyo, nimeonana na watu wa *African Development Bank*, nikawaambia milioni 600 kwa miaka mitatu ni milioni 200 kwa mwaka.

Nikawaambia Mradi wangu mmoja wa *North West* au wa *North East Grid* wa kuweka *transmission line* unahitaji Dola za Marekani milioni 700, mkinipatia milioni 700 inamaanisha kwa miaka mitatu nisije *ADB* kutafuta mkopo mwingine wowote. Ninadhani tunaenda nao vizuri huenda mwezi Machi wanaweza wakafanya maamuzi, Tanzania iwe kati ya nchi kumi ambazo zinaweza zikakopa Dola za Marekani bilioni 3.6. Kwa hiyo, tukizipata hizo hata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

Mheshimiwa Kafulila kule kwako umeme utasambaa utafika kila mahala. (*Makofi*)

Kwa kumalizia tu niseme, wengine wamekuwa na wasiwasi kwamba, fedha hazitafika. Mimi nataka kuwashakikisha kwamba, umeme vijijini nadhani ninyi nyote mnashuhudia kila mkoa hapa watu wanafungiwa umeme. Wizara yangu napenda kusisitiza tena labda pengine Wizara ya Nishati na Madini na Mashirika yake, mambo ya rushwa na wizi hayapo. Sisi hatufanyi kwa vyombo vyaya habari, tunawatoa kimyakimya tunawapeleka wanapofaa kupelekwa. Kwa hiyo, ninyi pitisheni huu Muswada kwa sababu hizi fedha zitaleta umeme vijijini. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninaomba niwashawishi Wabunge wenzangu, labda tukatishe mjadala tupitishe, twende mbele tuongee mambo mengine. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi pamoja na Wabunge wote, ambao wamechangia hoja hii kwa maandishi na kwa kuzungumza, lakini wengine nilikuwa nikiwaona kwa *body language* kwamba sote kimsingi tumekubaliana na pendekeso la Serikali. Nashukuru sana kwa hili. (*Makofi*)

Nami katika kuweka tu msisitizo, naomba niende katika kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, ni za msingi sana. Tunakubaliana nazo na nyingine kama hatujatoa majibu hapa, basi aidha tunakwenda kuzifanyia kazi, lakini tutakuwa tunatoa majibu kadiri ambavyo inawezekana.

Kwanza, naishukuru sana Kamati kwa mchango wao mkubwa katika kuhakikisha hili linafanikiwa. Tulikuwa pamoja muda wote na hadi tumefikia hapa, kwa mara ya kwanza Kamati ya Bajeti nadhani itakuwa imeweka rekodi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)]

kuwa na mkutano mdogo sana jana ambapo si zaidi ya dakika 25 tumemaliza mjadala, kwa sababu sote tulikuwa katika misingi ileile. *Specifically, kulikuwa kuna hoja ambayo imetoka Kambi ya Upinzani kuhusiana na ghamama ambazo zilitajwa; call back, call waiting na kadhalika.*

Kimsingi, huduma hizi hazijaingizwa katika kutoza kodi katika huduma moja moja. Kwa hiyo, kwanza, kuna zile ambazo wala hazijaingizwa katika *consideration* hii, lakini hiso ambazo zitakuwa *considered* kwa utaratibu huu ambaeo tumeuleta wa kuongeza *excise duty*, ghamama yake itakuwa ndogo sana. Kwa hiyo, kimsingi, kiujumla wake hatutaraji kwamba zitaongeza ghamama za matumizi.

Mheshimiwa Mbatia, umezungumzia vizuri kwamba, tu-*advance* hii *amount* na sisi tunakubaliana nalo, tunalichukua tunakwenda kukaa na wenzetu wa Benki Kuu ya Tanzania, kuona ni jinsi gani watatupatia ile *advance* bilioni 178 na kuweza *ku-facilitate* Miradi hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbatia na Mheshimiwa Shekifu, tunawashukuru sana kwa mawazo hayo.

Mheshimiwa Pamba, amezungumza vizuri kwamba, tuendelee kushirikiana na wadau katika kuhakikisha wigo wa kodi unapanuka, lakini kuhakikisha kwamba, kunakuwa hakuna hizi changamoto ambazo zimejitokeza. Labda hili tu nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kodi hii ni *mechanism* yake tu kukusanywa ndiyo ambapo tunailleta hapa. Kodi hii inapaswa kila mmoja wetu tuchangie, ni kodi hii pamoja na kodi nyingine. Kama tuko hapa tunahitaji maji, tunahitaji umeme na kweli tunasimama Wananchi wa Jimbo langu hawana hivi; hizi ndizo *mechanism*. Nadhani Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi tumeona jinsi Wananchi walivyo na mwamko wa kushiriki katika Miradi yao ya Maendeleo wana-*contribute* sana tu, wanachangia sana kwenye Miradi ya Maendeleo. Sisi Serikali tumerahisisha hiyo *contribution* ya Wananchi katika kuhakikisha kwamba, hii Miradi ya Maendeleo inafanikiwa.

Dunia ya leo hatuvezi kwenda pahali popote bila

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)]
ya mchango wa *private sector*. Ninaposema *Private Sector*
hana sikuudii makampuni.

Mheshimiwa Spika, nikitoka nje nikienda dukani leo ninakuwa ni *private sector*, yaani yule *individual* siendi pale kama Serikali. Kwa hiyo, vyovypote itakavyokuwa ni wajibu wa kila Mwananchi kulipia kodi. Kwa hiyo, hata kama utakuwa una-*earn* shilingi 500, *mechanism* ya kodi hii ni kwamba, utatumia thumni kwa sababu kipato chako ni 500, utatoa thumni utachangia maendeleo. Mwenye shilingi 10,000 atatoa shilingi 1,000 atachangia maendeleo. Kwa hiyo, kila *criteria* ya kipato, ukiwa una pesa ndogo utachangia kidogo na ukiwa unapata kipato kikubwa utachangia kikubwa; ndiyo *mechanism* ya kodi hii. Kodi haikufutwa ipo palepale. Tunatarajia kwamba, hii *mechanism* yake ya ukusanyaji tumei-easy tu kutokana tu na kipato cha mtu, kwa hiyo hili, tumelizingatia sana.

Lingine ni kiasi gani tumekusanya kwenye *post-paid*, kama nilivyosema kwamba, hii kodi ilipopendekezwa si kama sisi Serikali tulikuwa tumekaa tunasubiri tu, hapana, tulikuwa tunaanza kukusanya. Sasa *category* ya *post-paid* na *pre-paid* tulikuwa bado hatujai-*consider*, sisi tulikuwa tunakusanya kodi kwa ujumla wake. Taratibu za kukusanya kodi zilikuwa zinaendelea kama kawaida. Isipokuwa sote tunajua kwamba, yaliyotokea yametokea, lakini leo tunakuja kwa ajili ya kufanya marekebisho ili twende *smooth* kama ambavyo tulitarajia.

Mheshimiwa Rajab Mbarouk, hayupo lakini atakuwa amesikia, hatukushindwa na makampuni ya simu. Hilo naomba niliweke wazi; hatukushindwa wala hapa *statement* kama hizo nadhani zitakuwa zinaweka sasa *friction* baina ya Makampuni na Serikali. Katika *consideration* moja ya kulipia kodi ni *flexibility* tu. Hii kwa sababu tunataka tuweke wazi kwa pande zote mbili ndiyo tulikaa na makampuni ya simu, hatukushindwa. Yeye mwenye ame-*admit* kwamba, hata hiyo *judgement* walipokwenda kupeleka hiyo kesi, Serikali ilikuwa katika *position* nzuri tu na hilo limetokezea.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)]

Vipi Zanzibar watapata fedha hizi; kweli ushuru wa bidhaa ni katika moja ya mambo ya Muungano kama ilivyoelezwa katika Katiba, Toleo la 2005, Ibara ya (4), katika Nyongeza ya Kwanza. Kwa hiyo, Zanzibar kule, Ofisi za TRA zipo, zitakuwa zinakusanya ushuru huu kama ambavyo inakusanya ushuru mwingine wa *excise duty* katika mambo mengineyo. Sasa basi kwa sababu Zanzibar fedha kama hizi zinapokusanya zinaelekezwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika akaunti yao, kwa hiyo, kwa upande wa Zanzibar itajua fedha hizi zitaelekezwa wapi. Kwa hiyo, hili lipo wala halina matatizo yoyote.

Ameongelea kuhusiana na wanafunzi wataathirika labda kwa sababu ya matumizi ya *internet* na nini. Naomba tuliweke wazi jamani, hapa *consideration* yetu ni ya watu wote. Mwanafunzi hatoweza kusoma kama hana umeme, maana hata hiyo *internet* anayotaka kutumia hawezি kuitumia bila umeme. Kwa hiyo, cha msingi hapa tulipie ili sasa hayo mazingira mazuri ya mwanafunzi kusoma yapatikane. Mwanafunzi hataweza kusoma kama hakuna maji, kwa hiyo, tusiangalie tu upande mmoja. Hapa hasa tunataka kuweka mazingira mazuri ya kila mtu kufaidika na *infrastructure*, kama tunapeleka umeme vijijini ni pamoja na huyo mwanafunzi. Kwa kuwa vijijini sasa hivi hakuna *internet*, kwa nini hatuwezi ku-access *internet* ni kwa sababu hakuna umeme. Sasa hii kodi inampelekea yule aendeleee zaidi kwa kutumia. Kwa hivyo, hiyo haikuwa *justification* kabisa. Mheshimiwa Mbarouk, nadhani tumelewana hapo vizuri kabisa. (Makof)

Wengi tumeambiwa hapa tuangalie labda Afrika Mashariki, Rwanda, *eight percent*, kweli na Kenya *twelve percent* katika *excise duty*. Kwa nini ushuru wao unakuwa mdogo? Hili si la upande mmoja, kulipa kodi ni Mwananchi, ni Mfanyabiashara. Mimi leo kama ninakwenda dukani nanunua kitu sidai risiti, yule mtu atachukua ile hela ambayo ilikuwa ilipiwe kwa Serikali ilete maendeleo anamfaidisha Mfanyabiashara.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)]

Kwa wenzetu hawa wa Afrika Mashariki, jamani *mindset* zao zipo tafouti, ni kwamba, wanajua wajibu wao kama Mwananchi wa kulipa kodi. Akienda dukani, yaani *automatic* wala hauna haja ya ku-negotiate unatolewa risiti yako. Hapa ni tofauti; ameongea Mheshimwia Silinde, ukienda tu pale Mwananchi kweli *logic* inakuja, anakwambia labda simu bila risiti ninakuuzia kwa shilingi 100,000 na ukitaka na risiti ninakuuzia kwa shilingi 140,000. Haijawaki kutokea kweli tukawa Mwananchi adai kwamba hii ni haki yangu. Sasa angalau waulizie ule mchanganuo inakuwaje bila risiti uniuzie hivi, inakuwaje na risiti unaniuzia hivi! Kwa hiyo, ni wajibu wetu sote, huu si wajibu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna siku nilimsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja anasema, ye ye ham-*encourage* mtu kutumia *EFD*. Nilishangaa sana Mheshimiwa Mbunge unasema hum-*encourage* Mfanyabiashara atumie hili *EFD*. Sasa haya mapato tutayapata kutoka wapi? Ni wajibu wetu sote, kama Serikali tunaleta *proposal* lakini *implementers* ni sisi sote humu ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ufupi, nadhani tunakwenda vizuri, *signal* zote zinaonesha kwamba, Waheshimiwa Wabunge sote tumekubaliana na Muswada huu. Yale mawazo ambayo yametolewa yote ni *valid*, sisi kama Serikali tutayachukua tutakwenda kuyafanyia kazi ili kuhakikisha kwamba tunaboresha ukusanyaji wa kodi na bajeti yetu hasa ya ndani kama tunavyoendelea ita-improve.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote. Ninaomba kutoja hoja. (*Makofii*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushuru
wa Bidhaa wa Mwaka 2013 (*The Excise Management
and Tariff) (Amendment) Bill, 2013*)**

Jina Refu halina marekebisho.

Ibara ya 1

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.
WILLIAM A. MGIMWA, THE MINISTER FOR FINANCE DURING
THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE EXCISE
(MANAGEMENT AND TARIFF) ACT, 2013"**

Made Under S.O. 86(1)(b)

A Bill entitled "The Excise (Management and Tariff) Act, 2013" is amended:

A: In Clause 1 by-

- (a) Deleting the marginal note and substituting for it the following:
"Construction and commencement."
- (b) Re-designating section 1 as section 1(1);
- (c) Adding immediately after the re-designated subsection (1) the following new subsection:
"(2) This Act shall come into operation on the 1st day of January, 2014."

Dodoma,
....., 2013

WAM
MF

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ibara ya 2

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. EZEKIA
DIBOGO WENJE, MEMBER OF PARLIAMENT FOR
NYAMAGANA CONSTITUENCY AT THE SECOND READING
OF A BILL ENTITLED “THE EXCISE (MANAGEMENT AND
TARIFF) ACT, 2013”**

Made Under Standing Order 86(11) and 88(2)

A Bill entitled “The Excise (Management and Tariff) Act, 2013” is amended as follows:

A: In Clause 2 by deleting figure “17” appearing in subsection (3) **as amended by the Government** and substituting for it figure “14.5.”

**EZEKIA DIBOGO WENJE
NYAMAGANA CONSTITUENCY
21/12/2013**

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nimeleta marekebisho kwenye Ibara ya (2) ili isomeke kama ifuatavyo: *“In Clause 2 by deleting the figure “17” appearing in sub-section (3) as amended by the Government and substituting for it figure “14.5.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta haya marekebisho, naelewa umuhimu wa kukusanya kodi. Nimemsikiliza Mheshimiwa Profesa Muhongo kwa makini sana na nimemsikiliza Mheshimiwa Naibu Waziri mtoa hoja, ninaelewa umuhimu wa kukusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba, tunapoongeza hii kodi kutoka asilimia 14.5 kupeleka asilimia 17, wanaoenda kulipa hii kodi *actually in real sense* ni Wananchi. Pili, Serikali ilituahidi kwamba, itakapofika Desemba, 2013, watakuwa wameshaanzisha ule Mfumo wa *Traffic Monitoring System*. Takwimu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. EZEKIA D. WENJE]

zinaonesha kwamba, nchi ambazo ziliweka *Traffic Monitoring System* kama Ghana, mwaka 2009, mapato kutoka kwenye *Telecom Industry* yaliifika asilimia kumi ya Pato la Taifa.

Sasa uzembe wa Serikali wa kutoanzisha huu mfumo wa *Traffic Monitoring System*, bado unafanya mapato kutoka kwenye hii Sekta kushuka chini. Uzembe wa Serikali leo inataka kuongeza mzigo kwa wananchi. Nilipata *note* hapa nikaulizwa kwamba, *substitute* ya hiyo pesa ambayo unataka tupunguze itatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini *Traffic Monitoring System* kianza hata *by January 2014*, mapato kutoka kwenye hii *Telecom Sector* inaenda *ku-rise almost by more than ten percent* na hakuna haja ya kuwaongeza Wananchi mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo hoja yangu.

MWENYEKITI: Unajua kwa Muswada huu siyo Sheria ya kawaida, kwa sababu kama walishafanya hesabu *17 percent*, walifanya hesabu ndiyo hela itakayopatikana, utakapopunguza hiyo watatoa wapi nyingine katika kipindi hiki? Kanuni ile inasema hivyo, kwamba, unapobadilisha hapo lazima ulete hesabu *immediately*.

Mheshimiwa Naibu Waziri, nisikujibie, lakini kuna Kanuni, nilitaka kukumbusha hilo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninataka kutoa ufanuzi kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Wenje, anasema tuweke hiyo *14.5* kwa *ku-consider* kwamba *Traffic Monitoring System* itakuwa *installed*. Naomba kutoa taarifa kwamba, huu mtambo tayari umekwishakuwa *installed* na fedha itakayopatikana kutokana na huu mtambo tayari imo katika Bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, huo mtambo hautakwenda zaidi ya kile ambacho

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)]

tayari tumekichukua. Kwa hiyo, fedha zake zote tayari zimo katika Bajeti ya Serikali. Hii ni *mechanism* nyingine ambayo tunaandaa hapa. Ahsante.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila marekebisho yoyote)

Ibara ya 3

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila marekebisho yoyote)

(Bunge lilitrudia)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa wa Mwaka 2013 (The Excise Management and Tariff) (Amendment) Bill, 2013

(Kusomwa Mara ya Tatu)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kanuni 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa wa Mwaka 2013 (The Excise Management and Tariff Act, 2013), Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Namba 3 wa Mwaka 2013 (The Excise Management and

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)]

Tariff Act, 2013), kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoja hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ullisomwa*
Mara ya Tatu na Kupitishwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, tunaomba Serikali sasa ikafanye kazi ya kukusanya haya mapato. Kama tulivyosema na ninaiagiza Kamati yangu ya Bajeti na Serikali yenyewe. Unajua mabadiliko ya mfumo wa Bajeti tuliofanya, *unless* kuna mabadiliko mengine hayafanyi kazi. Kwa mfano, tunaanza tarehe 1 Julai, sasa tarehe 1 Julai kama hamjachukua hela za watu wengine mtatumia nini? Itakuwa mnasubiri kama tulivyofanya na ndivyo ilivyo sasa.

Naomba Wataalam wakalifanyie kazi. Wasiseme Wabunge walisema, Wataalam mkalifanyie kazi na linafanyika katika nchi nyingi. Mkayafanyie kazi haya mambo, haiwezekani tukawa tunapitisha tarehe 1 hakuna fedha; kumbe tulibadili nini sasa? Nawaombeni Mawaziri, mabadiliko yale yalikuwa makubwa na ni lazima yawe na mabadiliko mengine na mengine ni hayo.

Kwanza, ninaamini tukifanya hivyo, wale watakaosimamia ukusanyaji wa kodi hata Benki Kuu itasimamia kwa sababu ina hela zake. Mkiacha tu *TRA* wanasi mama na Hazina, wakikusanya haya, wakashindwa haya; lakini Benki Kuu mkichukua hela yao watawasimamia mrudishe yao. Kwa hiyo, jamani mkaangalie, mabadiliko yoyote yanahitaji mabadiliko mengine ambayo yanaunga mkono mabadiliko hayo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Sisi tunategemea hili litakuwa mwisho mwaka huu, mwaka mwingine tuanze kufanya kazi vizuri zaidi. Kwa hiyo, nawapongeza Kamati ya Bajeti na nawapongeza Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge, kwa kazi nzuri. (Makof)

Tunaendelea na hatua inayofuata, Katibu!

KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema, kwa kutufikisha salama siku ya leo. Tumekuwepo hapa Dodoma kwa takribani siku 15 za kazi ambapo tumeweza kutekeleza majukumu na kazi za Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge lako Tukufu ambapo tunahitimisha shughuli zilizopangwa hivi leo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii ya mwanzo kabisa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro, Mbunge, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu. Wengi wetu tunafahamu uwezo mkubwa wa Dkt. Asha-Rose Migiro na bila shaka ndiyo sababu Mheshimiwa Rais, alifanya uamuzi wa kumteua kuwa Mbunge kwa kuzingatia sifa nzuri alizonazo. Pamoja na kumpongeza, napenda kumtakia kazi njema ndani na nje ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, tangu Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wamepotelewa na ndugu, jamaa na marafiki. Napenda kutumia fursa hii kuwapa pole wote waliofikwa na misiba hiyo.

Katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge, walipata fursa ya kujadili Azimio la Bunge kuhusu kuungana na nchi ya Afrika Kusini, katika kuomboleza kifo cha mwasisi, mpinga ubaguzi wa rangi, Rais wa Kwanza Mweusi wa Afrika Kusini, Hayati Nelson Mandela, kilichotokea tarehe

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

5 Desemba, 2013. Wote tunakubaliana kwamba huu ni msiba mkubwa kwa dunia nzima na hasa kwa wale wanaomfahamu Mzee Mandela na historia yake. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuwakilisha vyema Watanzania wote katika msiba huu mkubwa wa Afrika na Dunia nzima. (*Makofii*)

Hotuba ya Mheshimiwa Rais alioitoa wakati wa mazishi ya Hayati Nelson Mandela tarehe 15 Desemba, 2013 pale Qunu Kijjini kwa Hayati, ilitosha kabisa kuitangaza Tanzania dunia nzima katika ushiriki wake kwenye harakati za ukombozi Barani Afrika katika Karne ya 20. Ninaamini kwamba, hiyo ni Historia ambayo haitafutika vizazi vingi vijavyo. Tutaendelea kumuenzi Mzee Mandela kwa kuiga na kufuata nyayo zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge waliweza kuuliza maswali ya msingi 170 na ya nyongeza 458 ambayo yote yalijibowi na Serikali. Aidha, maswali 17 ya msingi na 15 ya nyongeza yalijibowi kwa utaratibu wa Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuuliza maswali mazuri na Waheshimiwa Mawaziri kutoa majibu ya maswali hayo kwa umahiri mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na shughuli hizo za kawaida, Bunge lako Tukufu lilikamilisha kazi kubwa zifuatazo:-

(1) Bunge lilijadili na kukamilisha Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni wa mwaka 2013. (*The Referendum Bill, 2013*);

(2) Kujadili Taarifa mbili za Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta Mtambuka;

(3) Kujadili Taarifa mbili za Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia Fedha za Umma; na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

(4) Kujadili Taarifa tisa za Kamati za Bunge za Kisekta.

Aidha, Bunge lako Tukufu lilijadili kwa utaratibu wa Hati ya Dharura Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa wa Mwaka 2013 (*The Excise (Management and Tariff) (Amendment) Bill, 2013*).

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kujadili Taarifa hizo na kutoa maoni na ushauri kwa uwazi mkubwa na kwa kina. Mapendeleko na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge umepokelewa na Serikali na utazingatiwa kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika Mkutano wa Bunge wa 13, hali ya upatikanaji wa chakula nchini kwa ujumla imeendelea kuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi kufuatia mavuno mazuri ya msimu wa kilimo wa mwaka 2012/2013 katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Tathmini ya chakula na lishe iliyofanyika mwezi Oktoba na Novemba, 2013 katika maeneo yenye matatizo ya usalama wa chakula na lishe inaonesha kuwa jumla ya watu 828,063 wanakabiliwa na upungufu wa chakula na watahitaji msaada wa chakula wa tani 23,312 hadi ifikapo mwezi Februari, 2014.

Vile vile kati ya mwezi Julai na Novemba, 2013, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) ilitenga jumla ya tani 16,119 za chakula cha mgao kwa Halmashauri zenyе mahitaji ya chakula cha msaada. Hadi kufikia tarehe 16 Desemba, 2013, jumla ya tani 13,716 zilikwishachukuliwa na Halmashauri husika. Tani 2,402 zilikuwa hazijachukuliwa na Halmashauri za Mwanga, Babati, Igunga, Mpwapwa na Manyoni.

Nawaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya ambazo hazijachukua chakula hicho kufanya hivyo kabla ya tarehe 15 Januari, 2014. Ambao hawatakeleza maagizo haya, watachukuliwa hatua za kisheria na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kinidhamu. Nitumie nafasi hii kuwahakikishia wananchi kuwa Serikali itaendelea kusimamia upatikanaji wa chakula katika Halmashauri zenyе hali tete ya chakula kwa lengo la kubainisha idadi ya watu wenye uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kutokana na miezi hii kuwa katika kipindi cha mwisho wa msimu wa ununuzi wa mazao, kiasi cha mazao yanayoingia sokoni kimeanza kupungua. Hali hii imesababisha bei za wastani za vyakula hasa mahindi na mchele katika soko hapa nchini kuanza kupanda ingawaje siyo kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, bei ya mahindi Kitaifa imepanda kutoka Sh.536.86 kwa kilo mwezi Oktoba, 2013 hadi kufikia Sh. 538.26 kwa kilo mwezi Novemba, 2013. Kwa upande wa Mchele, bei ya wastani wa Kitaifa imepanda kutoka Sh. 1,188.60 kwa kilo mwezi Oktoba, 2013 hadi Sh. 1,191.10 kwa kilo mwezi Novemba, 2013.

Pamoja na kuwepo kwa hali ya kupanda kwa bei, bado bei za sasa kwa baadhi ya mazao mfano mahindi, mchele, maharage na viazi ziko chini ikilinganishwa na zile za kipindi kama hiki mwaka jana. Natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa yenye mavuno mazuri kuendelea kuwahamasisha wakulima kuhifadhi chakula cha kutosha kwa mahitaji ya Kaya zao na kuuza ziada katika Soko ili kusaidia kupunguza bei ya vyakula katika Miji, hasa Miji mikubwa. Halmashauri zihakikishe kuwa zinadhibiti ununuzi holela wa chakula kutoka mashambani na majumbani mwa wakulima kwa lengo la kujihakikishia upatikanaji wa chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) ilipanga kununua tani 250,000 za nafaka. Wakala umeendelea na kazi hiyo na hadi kufikia tarehe 11 Desemba, 2013, Wakala ulikuwa umekwishanunua kiasi cha tani 218,499 za nafaka sawa na asilimia 87.4 ya kiasi kilichopangwa kununuliwa. Vile vile hadi kufikia tarehe 16 Desemba, 2013, Maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula yalikuwa na akiba ya jumla ya tani 233,808 za nafaka. Kati ya hizo, tani 233,315 ni za mahindi na tani 493 ni za mtama.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Wakati huo huo, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula unaendelea kuhamisha chakula kutoka katika maghala yake yaliyoko katika Mikoa iliyozalisha ziada kwenda kwenye maghala yaliyoko kwenye Mikoa yenyе upungufu wa chakula ili kukabiliana na mahitaji ya chakula cha msaada kitakachohitajika kusambazwa kwa walengwa. Hadi kufikia tarehe 9 Desemba, 2013, jumla ya tani 44,129 za mahindi zimeshahamishwa. Serikali inaendelea kuhamasisha wafanyabiashara kununua chakula katika Mikoa yenyе ziada ya chakula na kukipeleka katika Mikoa yenyе upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Serikali ilichapisha jumla ya vocha 2,796,300, kwa ajili ya pembejeo za kilimo kwa msimu wa kilimo wa 2013/2014. Hadi kufikia tarehe 12 Desemba, 2013, tani 74,925 sawa na asilimia 96 za mbolea ya kupandia na tani 42,295 sawa na asilimia 91 ya mbolea ya kukuzia, zilikuwa zimeshafikishwa katika Mikoa husika kulingana na aina ya mazao yanayohitaji mbolea hizo. Aidha, Maghala ya Wakala wa Mbolea Jijini Dar es Salaam yana akiba ya kutosha ya mbolea hiyo. Nirejee kutoa wito kwa Wakuu wote wa Mikoa kuhakikisha kuwa vocha zote zinatolewa kwa walengwa kwa wakati sambamba na aina ya pembejeo inayomlenga Mkulima husika kwa kuzingatia utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2013/2014, Serikali ilitenga jumla ya Shilingi bilioni 109.6 kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) kwa ajili ya kununua tani 250,000 za nafaka. Hadi kufikia tarehe 19 Desemba, 2013 *NFRA* ilikuwa imenunua jumla ya tani 218,499 zenye thamani ya Shilingi bilioni 109.25 na kwa ajili hiyo.

Kutokana na Serikali kutoa bei nzuri ya wastani wa Sh. 500/= kwa kilo ya mahindi, zoezi hilo lilikuwa na matokeo mazuri katika msimu huu kulinganisha na miaka iliyopita na liliwavuta wananchi wengi kupeleka nafaka katika Vituo vya kununulia nafaka. Hadi sasa Serikali imeshatoa Shilingi bilioni 100.6 kwa ajili ya zoezi hilo na imehakikisha kuwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Wananchi wote waliouza nafaka zao kwa *NFRA* wamelipwa fedha zao. Aidha, natambua kuwa *NFRA* ilitumia baadhi ya Wakala kukusanya nafaka hiyo kutoka kwa wakulima. Kama nilivyosema katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Serikali inatambua kuwa Wakala hao kutoka Mikoa ya Arusha, Dodoma, Njombe, Shinyanga, Ruvuma, Rukwa na Tanga wanaidai Serikali jumla ya Shilingi bilioni 8.65. Nawaomba Wakala wote wanaoidai Serikali kuendelea kuwa na subira kidogo wakati Serikali inaendelea na utaratibu wa kulipa fedha hizo mapema inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Desemba, 2013 Serikali ilizindua Mpango wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Kifedha, yaani *National Financial Inclusion Framework*. Uzinduzi wa Mpango huu ulifanywa na Malkia wa Uholanzi, Mheshimiwa Máxima Zorreguieta Cerruti ambaye pia ni Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Mpango wa Huduma Jumuishi za Kifedha na kushuhudiwa na Makamu wa Rais - Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Wawakilishi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, lengo la mpango huo ni kusimamia ukuzaji wa huduma za kifedha kwa jamii nchini na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili Sekta ya Fedha. Vilevile, Mpango unalenga kusogea huduma karibu kwa jamii pana zaidi ya Watanzania kwa kutumia mifumo ya Teknolojia mbalimbali katika kufikisha huduma za kifedha kwa wananchi na hasa Wakulima, Wafugaji na Wavuvi waliopo Vijijini ambaeo wengi wao wako nje ya mfumo rasmi wa kifedha.

Teknolojia hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Huduma za Kibenki za moja kwa moja na kupitia Wakala (*Agent Banking*);

(ii) Huduma za kifedha kupitia Mitandao mbalimbali kama vile *M-PESA*, *TIGO PESA*, *AIRTEL MONEY* na *Easy PESA*; na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

(iii) Vituo vya malipo kwa kutumia Wakala (*Point of Sales – POS*).

Aidha, Mpango huu utaweka mazingira linganifu na yaliyo bora kwa kutumia Sayansi na Teknolojia kutekeleza Sera ya Fedha kwa ufanisi, kuimarisha Sekta ya Fedha katika Pato la Taifa na kukuza uchumi kwa ujumla. Mpango huu pia utawezesha kuongeza kasi ya upatikanaji wa chakula, masuala ya lishe na maendeleo Vijijini kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia katika nchi mbalimbali Barani Afrika unaonesha kuwa watu wanaonufaika na mfumo rasmi wa Taasisi za Kifedha ni asilimia 24 tu. Kwa upande wa Tanzania, wananchi walipo kwenye mfumo rasmi wa Asasi za Kifedha ikijumuisha wale waliojiunga na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOs*) ni Asilimia 22. Asilimia 78 ya Watanzania wapo nje ya mfumo wa kifedha na wengi wao ni kutoka Vijijini hasa wakulima wadogo. Mpango huu wa Huduma Jumuishi za Kifedha unalenga kufikia asilimia 50 ya watu wazima wanaotumia huduma rasmi za kifedha ifikapo mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, kiwango hiki kidogo cha Wananchi walio katika mfumo rasmi wa huduma za kifedha unatokana na changamoto mbalimbali na ninaomba nizitaje baadhi.

(i) Miundombinu ya kuanzisha huduma za Kifedha Vijijini ni hafifu na hasa barabara, mawasiliano, makazi na huduma za kiusalama;

(ii) Wananchi wengi wa Vijijini bado hawajahamasishwa kutambua umuhimu na faida ya huduma za kifedha. Vilevile utamaduni wa kujiwekea akiba na kukopa ni mdogo; na

(iii) Taasisi nyngi za kifedha zinaogopa kwamba wananchi wengi wa Vijijini ambao ni wakulima hawana fedha za kutosha kuweza kuweka akiba katika Taasisi hizo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

na uwezo wao wa kukopa mikopo ni mdogo. Hivyo wakipeleka huduma zao huko, hawatapata faida.

Mheshimiwa Spika, lakini zipo faida nyingi za kueneza huduma jumuishi za kifedha kwa wananchi wengi wa Vijijini hasa wakulima, wafugaji, wavuvi na wajasiriamali wadogo. Miiongoni mwa faida hizo ni pamoja na:-

(i) Kuwezesha wananchi kujivekea akiba na pia kupata mikopo ya kuwawezesha kuanzisha miradi ya maendeleo na shughuli nyingine za kijamii;

(ii) Huduma za kifedha Vijijini zinawawezesha wananchi wengi hasa wakulima, wafugaji, wavuvi na wajasiriamali kupata mikopo ya pembejeo na mikopo ya ununuvi wa mazao;

(iii) Huduma za kifedha Vijijini ni Mkombozi wa makundi maalum kama vile Vijana, wanawake, wazee, na walemovu. Aidha, zinasaidia Wananchi kujiongezea kipato, kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ya Kilimo na kuongeza thamani ya mazao ya aina mbalimbali; na

(iv) Kuwepo kwa huduma za kifedha Vijijini kunaongeza usalama wa chakula, kulinda mazingira na kufanya Vijiji kuwa ni sehemu nzuri ya kuishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeonesha juhudini kubwa katika kuanzisha huduma jumuishi za kifedha nchini kwa mfano tumeweza kuanzisha Benki nyingi nchini. Tayari tunazo Benki takriban 52 zenye matawi zaidi ya 609 kote nchini. Lakini pia tunazo huduma za Bima kwa Makampuni Binafsi zaidi ya 27 na Mawakala wa Bima takriban 600. Ipo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Umma, mitano; Masoko ya Mitaji na Vikundi na Taasisi ndogo ndogo za Fedha (*SACCOS*) takriban 5,600. Aidha, tunazo huduma za kifedha kwa kutumia huduma za kifedha kuititia mtandao (PESA - MTANDAO) na Vituo vya Malipo kwa kutumia Wakala (*POINTS OF SALES - POS*). Inakadiriwa kuna Mawakala na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Vituo zaidi ya 55,000 ambapo waajiriwa wa moja kwa Moja (*Direct Employment*) wanakadiriba kufika takriban 100,000.

Mheshimiwa Spika, maisha bora kwa kila Mtanzania ni pamoja na kutumia Teknolojia na kurahisisha maisha. Kwa mfano, huduma za *M-PESA* peke yake zinawezesha malipo kwenye biashara mbalimbali zaidi ya aina 300 ikiwemo manunuzi kwenye *Supermarket* na maduka ya kawaida. Huduma hizo ambazo zinatolewa pia kwa njia ya *TIGOPESA*, *AIRTEL MONEY*, *EASY PESA* zinawezwa kulipia Luku, ada za shule na Vyuo, tiketi za ndege, kufanya marejesho Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, na kadhalika. Aidha, baadhi ya Makampuni haya yameunganisha huduma zao na Benki zaidi ya 20 ikiwemo *CRDB*, *NMB*, Benki ya Posta, *Standard Chartered*, *Amana Bank* na *Diamond Trust Bank (DTB)*. Vilevile, kwa kutumia huduma za jumuishi za kifedha, mteja anaweza kuhamisha fedha kutoka akaunti ya Benki kwenda *M-PESA*, *TIGO PESA* na kadhalika, halafu akazitoa kupitia Wakala. Kwa sasa Watumishi walio Vijijini hawana tena sababu ya kufunga Ofisi kufuata mishahara Benki, bali kupitia huduma hizi za Kifedha na wanaweza kutoa pesa kupitia Wakala, na kwa kufanya hivyo ufanisi na tija kwa Watumishi unaongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunayo kazi kubwa ya kutekeleza dhana ya Huduma Jumuishi za Kifedha Nchini. Lakini ni ukweli kuwa uzinduzi wa Mpango wa Kitaifa wa Huduma Jumuishi za Kifedha una manufaa makubwa na mengi ikiwemo kuongeza kasi ya Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini kwa kupeleka maendeleo Vijijini, kuongeza akiba ya chakula na pia kufikia malengo ya Milenia. Ni matumaini yangu kwamba uzinduzi wa Mpango huu utatuwezesha kusonga mbele kwa kasi kubwa zaidi. Natoa wito kwa Mabenki, Taasisi za Kifedha na Vituo vya Fedha kupitia mitandao (PESA MTANDAO) na Vituo vya malipo kwa kutumia Wakala kuongeza jitihada katika kusambaza huduma za Kifedha Vijijini ambako ndiko kwenye kundi kubwa la wananchi wanaohitaji huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wananchi wengi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

wanafahamu, Serikali kuititia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa mitambo ya kusafishia Gesi Asilia katika maeneo ya Madimba, Mtwara Vijijini na Songo Songo Wilayani Kilwa. Pia ujenzi wa Bomba la kusafirishia Gesi hiyo kutoka Mtwara na Songo Songo hadi Dar es Salaam unaendelea vizuri. Mradi huu utakapokamilika utaunganisha maeneo yanayozalisha Gesi Asilia hususan Mnazi Bay-Mtwara, Songo Songo, Kisiwani, Mkuranga, Ntorya na maeneo yaliyogunduliwa Gesi katika eneo la bahari ya kina kirefu. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa Gesi Asilia mbali na matumizi mengine, inatumika katika kuzalisha umeme ambaao kwa sasa asilimia kubwa unazalishwa kwa kutumia nishati ya mafuta yanayoingizwa kutoka nchi za nje na hivyo kuligharimu Taifa kiasi kikubwa cha fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mradi huu, kazi zifuatazo zimekamilika hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2013:-

(1) Kukamilika kwa upakuaji wa Shehena ya Sita ya Mabomba ya Mradi yapatayo 4,444 ya umbali wa Kilomita 51.169 katika Bandari ya Mtwara. Jumla ya mabomba yaliyowasili Nchini hadi Novemba, 2013 ni 24,935 ya umbali wa kilomita 295.5;

(2) Kusafisha Mkuza wa Mabomba, tayari Kilomita 498.5 zimekamilika;

(3) Usafirishaji wa mabomba kutoka kwenye yadi za kuhifadhi na kuyasambaza kwenye Mkuza tayari kwa kuyaunganisha kwa kuchomelea. Hadi sasa mabomba ya Kilomita 186.9 yamekwishasafirishwa;

(4) Uchimbaji wa njia ya kuweka bomba, yenye umbali wa Kilomita 27.0 umekamilika;

(5) Uwekaji wa mabomba kwenye njia yake sambamba na kuweka Mkongo wa Mawasiliano (*Fiber Optic Cable*) umekamilika Kilomita 21.1;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

(6) Kufukia bomba pamoja na Mkongo wa Mawasiliano. Tayari Kilomita 7.30 za Bomba pamoja na Mkongo wa Mawasiliano zimefukiwa; na

(7) Utafiti wa njia ya Bomba la Baharini nao umekamilika.

Mheshimiwa Spika, hayo ni maeneo machache ambayo nimeona niyaeleze kwa Watanzania katika maelezo yangu ya leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kazi za mradi huu ni kubwa lakini kwa ujumla zinaendelea vizuri na kwa kasi ya kuridhisha. Moja ya faida za mwanzo za mradi huu ambazo tumeziona ni pamoja na upatikanaji wa ajira kwa Wafanyakazi wa Mradi ambao sehemu kubwa ya ajira ni ushirikishwaji wa wazawa katika Mradi wa Gesi na Mafuta. Kwa kuwa kazi za ujenzi wa mitambo na Bomba la Gesi ni za kitaalamu sana, malengo ya Shirika la Petroli Nchini (*TPDC*) ni kuajiri wafanyakazi Wakiwemo Wazawa mapema ili waweze kushiriki na kujifunza kwa vitendo shughuli zote zinazohusiana na ujenzi wa mitambo na Bomba la Gesi hatua kwa hatua, tangu mwanzo hadi mwisho wa ujenzi. Utaratibu huu utasaidia kupata wataalamu wazuri na wazoefu wa Kitanzania watakaoendesha (*operations*) na kufanya matengenezo (*Maintenance*) ya mitambo na Bomba la Gesi kwa kipindi chote cha matumizi.

Mheshimiwa Spika, vilevile moja ya makubaliano katika Mkataba wa utekelezaji wa Mradi huu, Mkandarasi anawajibika kuwapeleka wafanyakazi kwenye mitambo na mabomba yanayofanya kazi kwa sasa kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja ili wajifunze pia kwa vitendo na kwa nadharia shughuli zote za kuendesha mitambo ya kusafisha Gesi Asilia na Bomba la Gesi. Malengo ya *TPDC* ni kuwapeleka wafanyakazi husika kwa awamu tofauti tofauti wakati wa kipindi cha ujenzi ili ikifika kipindi cha kukabidhi mradi wafanyakazi wote wawe wamekwishapata uzoefu wa kutosha.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, Kampuni nyingi zilizopo Mtwara zinazojishughulisha na mambo ya utafiti na uzalishaji wa Gesi na Viwanda vnavyohusiana na matumizi ya Gesi, zimekuwa zikisomesha na pia kuajiri wazawa. Kwa mfano, Mpango wa kujenga mitambo ya kutengeneza Gesi kuwa kimiminika (*LNG*) wa Kampuni ya *British Gas Tanzania* utakuwa na utengenezaji wa ajira nyingi za kiwango kuanzia Kada ya Chini na Kada ya Kati ambayo itasomesha Watanzania kupitia *VETA* katika fani mbalimbali. Wako watakaosomeshwa katika fani ya Vyuma, wengine ujenzi, uhandisi wa miundombinu na ufundi wa vyuma na umeme.

Katika Kada ya Kati, Kampuni ya Gesi Tanzania wanatarajiwa kusomesha wataalamu 16,756 waliofaulu vizuri masomo ya Kidato cha Nne. Takwimu zinaonesha kuwa kwa Mtwara tu, kumekuwapo ajira mpya 400, na Watanzania wanaotoa huduma mbalimbali kwenye Kampuni za Gesi na Mafuta ni sawa na asilimia 70 ya watoa huduma hiyo nchini. Asilimia 30 iliyobaki ya watoa huduma inatolewa na Wageni.

Katika kada za juu, Kampuni itasomesha na kuajiri wataalamu wa Jiolojia, Uhandisi, Kemia na Sayansi husika kwenye Gesi na Mafuta. Matokeo yameanza kuonekana ambapo jumla ya wanafunzi wa *VETA* 370 wamesomeshwa kuhusu Gesi na Mafuta kwa kiwango cha cheti cha Kimatalifa na Wanafunzi 12 wa kada za juu wamepata ufadhilli na wanasomea fani za Gesi na Mafuta ndani na nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Kampuni ya *British Gas Tanzania* wamegundua gesi kiasi cha futi za ujazo trillioni 13. Katika kuandaa na kuendesha mradi wa uzalishaji Gesi nyingi kiasi hicho ni dhahiri kwamba ajira zitapatikana kwa maelfu ya Watanzania. Katika hatua ya ujenzi, mradi utatoa ajira kwa maelfu; na katika uzalishaji vile vile ajira nyingine zaidi zitapatikana hapa nchini, na katika mnyororo wa usambazaji, ajira zaidi zitajitokeza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapa Watanzania matumaini, kwamba Mradi wa Gesi nchini una manufaa mengi sana, kuanzia upatikanaji wa Gesi na Ajira kwa wazawa. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu manufaa ya mradi huu katika nchi yetu. Ni fursa ya kipekee ambayo wananchi wetu wanatakiwa wafaidike nayo katika kuwaletea maisha bora.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Serikali ililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu mikakati mbalimbali itakayoteklezwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Ndani. Moja ya hatua hizo muhimu ni kuendelea kuimarisha matumizi ya mashine za kielektroniki za kutoa risiti (*Electronic Fiscal Devices - EFDs*). Mashine hizi zimeunganishwa kwa mtandao wa Kompyuta moja kwa moja na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa lengo la kuwezesha Serikali kupata mapato stahiki bila udanganyifu. Vilevile mashine hizi zinasimamiwa kupitia mtandao wa kielektroniki ambapo hupeleka taarifa moja kwa moja kwenye Hifadhi Kuu ya Kumbukumbu za Mamlaka ya Mapato Tanzania kila siku.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa zoezi hili kwa mwaka huu, Serikali imelenga kuingiza walipa kodi 200,000 kati ya 1,500,000 ili waweze kutumia mashine za kielektroniki. Walengwa wa utaratibu huu ni wafanyabiashara wenye biashara kubwa zenyе mtaji wa kati ya Shilingi milioni 14 na Shilingi milioni 40. Katika zoezi hili, wafanyabiashara wadogo wanaoendesha biashara zisizo rasmi kama vile Wamachinga na wale wanaotembeza bidhaa barabarani na Mama Lishe hawahusiki na utaratibu huu hata kidogo. (*Makofj*)

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa zoezi hili kumejitokeza malalamiko kutoka kwa baadhi ya wafanyabiashara nchini hususan wa Mikoa ya Mbeya, Morogoro, Lindi na Dar es Salaam (Kariakoo) kuhusiana na bei na matumizi ya mashine hizi. Malalamiko makubwa ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Wafanyabiashara hao ni kuhusu: Bei kubwa ya ununuzi wa mashine za kielektroniki; bei kubwa ya karatasi za kutolea risiti; mchakato uliotumika kununua mashine za kielektroniki; walengwa wa kutumia mashine hizo; na gharama za matengenezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maendeleo ya sayansi na teknolojia ya mawasiliano ya kisasa (*ICT*); wataalam wanathibitisha kwamba, mashine za kielektroniki zinafanya kazi zifuatazo:-

(1) Zinatoa risiti na ankara za kodi kwa urahisi na mfanyabiashara huondokana na adha ya kuchapisha au kununua vitabu vingi vya kuandika risiti ambavyo utunzaji wa nakala zake unaleta usumbufu;

(2) Zina uwezo mkubwa wa kutunza kumbukumbu za mauzo, manunuzi na mali za Biashara (*stock*) bila kufutika kwa muda usiopungua miaka mitano;

(3) Mtumiaji anaweza kutoa kwa urahisi taarifa za mauzo yake kwa siku, kwa wiki, kwa mwezi, kwa mwaka na kwa wakati wowote kwa kipindi kisichopungua miaka mitano;

(4) Humwezesha mfanyabiashara kutuma taarifa zake za mauzo moja kwa moja kwenda Ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na Mamlaka nyingine zenye mahitaji ya taarifa hizo, kama vile Taasisi ya Taifa ya Takwimu, Benki Kuu, *EWURA* na *SUMATRA*;

(5) Mashine zinaweza kupokea maelekezo moja kwa moja kutoka kwenye Mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, na kumtaarifu mfanyabiashara taarifa yoyote ya kodi inayomhusu;

(6) Kutuma na kupokea fedha kwa njia ya "*Mobile Money*". Utaratibu huu unamwezesha mtumiaji kutumia mashine hizi kulipia kodi na huduma nyingine moja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kwa moja kama vile, ankara za umeme, maji, simu, na kadhalika;

(7) Mashine za Kielektroniki zinatumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza inayoelewaka kwa wananchi wengi; na

(8) Mashine za Kielektroniki zinaiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kutambua mauzo sahihi ya mfanyabishara na hivyo kuweza kutoza kodi halali.

Mheshimiwa Spika, msingi wa bei ya kununulia mashine hizi za kielektroniki umezingatia pamoja na mambo mengine, manufaa na faida nyingi nilizozitaja kwa mtumiaji na vilevile upande wa Serikali na ubora wa mashine zenyewe. Aidha, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika nchi mbalimbali duniani, unaonesha kuwa mashine zenyewe ubora unaokidhi mahitaji niliyoyataja hapo juu, zinauzwa na wasambazaji kwa katи ya Sh. 600,000/= (Dola 375) hadi Sh. 778,377/= (Dola 486) ikilinganishwa na bei za Mashine za Kielektroniki za nchi nyingine zinazotumia mfumo unaofanana na wa Tanzania ambazo zinauzwa bei kubwa za katи ya Dola za Kimarekani 360 hadi 870. Pamoja na bei hizo, Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea kujadiliana na wasambazaji wa mashine hizo ili kuona uwezekano wa kushusha bei hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei za karatasi za kutolea risiti, uchunguzi unaonesha kuwa karatasi hizo zinauzwa katи ya Sh. 2,200/= hadi Sh. 4,500/= kuzingatia ubora na ukubwa mbalimbali wa risiti hizo. Karatasi hizo zina uwezo wa kutoa wastani wa risiti katи ya risiti 200 hadi 1,000 kulingana na urefu wa "Paper Roll" au bunda. Bei ya karatasi hizo zinazojulikana kama "Thermal Paper" umezingatia kwamba ni za kisasa na hazifutiki kwa urahisi na zina alama za siri ndani yake kwa ajili ya kuongeza usalama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu uliotumika kuwapata watengenezaji na wasambazaji wa mashine hizi za kielektroniki na wasambazaji wa karatasi, napenda

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kulifarifu Bunge lako Tukufu kuwa ulikuwa wa wazi na wa ushindani wa Kimataifa na haukuwa na dosari yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta watengenezaji na wasambazaji kwenye Awamu ya Kwanza watengenezaji wanne na wasambazaji sita walipatikana kwa kutumia Zabuni ya wazi ya Kimataifa (*International Competitive Tendering*) kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005. Kuanzia mwezi Desemba, 2009 mpaka Mei, 2010 makubaliano yaliingiwa kati ya kila Mtengenezaji na Msambazaji aliyechaguliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) chini ya "*Memorandum of Understanding (MOU)*".

Kwenye Awamu ya Pili ya utekelezaji wa utaratibu huohuo wa Zabuni ya Watengenezaji ilitangazwa kwenye gazeti la *Daily News*, *The African*, Tovuti ya *TRA* na Tovuti ya *PPRA*. Jumla ya Wazabuni 14 walituma maombi ambayo yalifunguliwa mara moja baada ya saa 4.00 asubuhi tarehe 27 Septemba, 2012. Watengenezaji wa Mashine wanne walichaguliwa kati ya 14 waliokuwa wameomba na Wasambazaji watano walipatikana kati ya tisa walituma maombi yao ndani ya muda. Kwa kifupi, huo ndiyo utaratibu uliotumika ambao ulikuwa wa wazi na ushindani.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha ubora wa mashine hizi za Kielektroniki, Watengenezaji wametoa dhamana ya muda wa miaka mitatu kwamba mashine inayoharibika bila kkusudia na watawajibika kutoa mashine nyingine na pia kutoa elimu ya matumizi ya mashine hizo. Vilevile, kwa mujibu wa Mkataba ulioingiwa kati ya Wasambazaji na *TRA*, Wasambazaji wanawajibika kuzifanyia matengenezo mashine hizo kila zinapoharibika ili kuondoa usumbufu kwa watumiaji kutafuta watengenezaji wao wenyewe. Napenda kuwashakikisha wafanyabiashara na wananchi wote kwamba, utaratibu wa kutumia mashine hizi haukuwekwa kwa nia mbaya, bali unalenga kumrahisishia mfanyabiashara kutunza kumbukumbu za kila siku za biashara na kuwawezesha kulipa kodi stahiki Serikalini.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa mashine hizi katika kuongeza mapato ya ndani; na ili kuyashughulikia malalamiko ya baadhi ya wafanyabiashara yaliyojitekeza, Serikali ilisogeza muda mbele hadi mwisho wa mwezi huu Desemba, 2013 ili kuona namna ya kuweza kutoa elimu ya kutosha na kuafikiana. Lengo ni kuwawezesha walengwa kupata nafasi zaidi ya kuijandaa kununua mashine hizi na kujifunza namna ya kuzitumia. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa Sekta Binafsi inaendelea kutoa elimu kuhusu matumizi endelevu na faida za Mashine za Kielektroniki kwa wafanyabiashara na wanunuzi wa bidhaa na huduma. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa ngazi zote kushirikiana na Serikali, kuwaelimisha wananchi na Wafanyabiashara kuhusu manufaa ya mfumo huu wa jambo hili ili kwa pamoja tuweze kuhakikisha kwamba Taifa letu linakusanya kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 - 25 Oktoba, 2013 nilifanya ziara ya kikazi nchini China kufuatia mwaliko wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Watu wa China Mheshimiwa Li Keqiang. Katika ziara hiyo, nilifuatana na Viongozi wa Serikali wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wabunge, Viongozi wa Asasi za Sekta Binafsi Tanzania na Watendaji mbalimbali kwa ajili ya kujumuika nami katika ziara hiyo.

Dhamira kubwa ya ziara hiyo kimsingi ilikuwa: kukuza mashirikiano ya kibiashara na utalii nchini; kufanya mazungumzo na vyombo vya fedha; kuendeleza uhusiano wa nchi hizi mbili; kuona Sekta Binafsi ya Tanzania inavyoweza kushirikiana na wenzetu wa China na mwisho kutoa shukrani kwa misaada na mikopo ambayo nchi yetu imepokea kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

Mheshimiwa Spika, kwa makusudi katika ziara hiyo, niliwachukua viongozi wa *Private Sector Foundation* (Baraza la Sekta Binafsi), Katibu Mtendaji, Mzee Reginald Mengi pamoja na Katibu Mtendaji kuambatana name

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

katika ziara hiyo ili waweze kwa pamoja kutumia fursa hiyo ya ziara kujenga mahusiano na Sekta Binafsi kutoka China.

Mheshimiwa Spika, Taifa la Jamhuri ya Watu wa China limepiga hatua kubwa na tumeweza kujifunza mambo mengi. Kutohakana na maendeleo hayo makubwa yaliyotokea katika Taifa la China, naomba nitoe wito wa kuwakaribisha ili kushirikiana na Tanzania na Bara la Afrika kwa ujumla katika nyanja za kiuchumi, utamaduni na kisiasa. Yapo maeneo mengi ya ushirikiano, na mimi naamini tukitumia vizuri fursa hiyo, yako mengi ya kujifunza.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo nilipata fursa ya kutembelea Miji mikubwa nchini China na kukutana na Viongozi mbalimbali na kubadilishana nao mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ziara hii ilikuwa ya mafanikio, tumeweza kujenga na kudumisha ushirikiano ambao upo kati ya nchi hizi mbili ambao ulijengwa tangu miaka ya nyuma baina ya Hayati Baba wa Taifa - Mwalimu Julius Nyerere pamoja na Mwenyekiti Mao Zedong wa Jamhuri ya Watu wa China. Kwa upande mwingine, tumeweza vile vile kukutana na makampuni mengi yapatayo 30 na kufanya mazungumzo nao na wengi wameitikia wito wa kuja kutafuta fursa za uwekezaji hapa nchini. Naamini tukijipanga vizuri tunaweza kutumia fursa hiyo vizuri sana kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo niliweza vile vile kushiriki katika utajji wa saini na Mikataba mbalimbali baina ya China na Tanzania katika maeneo mbalimbali ya Sayansi, Teknolojia, pamoja na Utalii. Mikataba mingine iliyotiwa saini ni uuzaaji wa bidhaa za baharini za Tanzania nchini China na kuanzisha Ukanda wa Kisasa wa Viwanda vyta Nguo pamoja na kukuza zao la Pamba nchini. Pia tulisaini Mikataba ya Maelewano inayohusu Sekta ya Nishati, Nyumba na Makazi baina ya Makampuni ya China na Mashirika yetu ya Umma yakiwepo Kampuni ya Umeme -

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

TANESCO, Shirika la Taifa la Maendeleo - NDC na Shirika la Taifa la Nyumba - NHC.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ya ziara hiyo ni pamoja na kuyashawishi Makampuni makubwa ya usafiri wa anga na Mawakala wa safari za kitalii kuwekeza Tanzania. Katika jitihada hizo, nilikutana na Makampuni ya China Hainan, *China Southern Air Line Holding Company* na *China Travel Service (Holdings) Hong Kong Limited*.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Makampuni haya ya Usafiri wa Anga ya nchini China yameonesha utayari wao wa kuanzisha safari za ndege za moja kwa moja kati ya Tanzania na China. Aidha, Kampuni ya *China Travel Service (Holdings) Hong Kong Limited* ambayo inafanya biashara ya kusafirisha watalii katika nchi mbalimbali duniani, wameonesha nia ya kuja kuwekeza hapa nchini katika Sekta ya Hoteli kubwa za Kitalii. Kampuni ya *China Merchants Holdings International Limited* ambayo imehusika katika ujenzi wa Bandari kubwa na Mji mkubwa wa Shenzhen katika Jimbo la Guangdong. Kwa upande wake imekubali kuingia ubia na Serikali yetu katika ujenzi na kuendeleza Bandari mpya ya Bagamoyo na Mji wa Bagamoyo unaotarajiwa kuwa "Trade Hub" ya Afrika. (Makofii)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba mniruhusu niongeze dakika chache mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapomaliza hotuba yake. (Makofii)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, unaweza kuendelea.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imedhamiria kuendeleza uchumi wake kwa lengo la kufikisha Tanzania kuwa Nchi ya Uchumi wa Kati kabla au ifikapo mwaka 2025. Viashiria vyote vinaonesha hivyo, na ndiyo sababu Makampuni yote niliyoyazungumza hapa yamedhamiria

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kuja kuwekeza hapa nchini. Noamba nitoe wito kwa mara nyingine kwamba wafanyabiashara hapa nchini watumie nafasi hii kujaribu kujenga mahusiano hayo mapya na kushirikiana nao katika kufanya biashara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Novemba, 2013 Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alihutubia Bunge lako, ambapo pamoja na mambo mengine alizungumzia suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki na mustakabali wa Tanzania katika Jumuiya hiyo. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba katika Mkutano Mkuu wa 15 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2013 Kampala nchini Uganda, Wakuu wa Nchi hizo akiwemo Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete walikutana na waliidhinisha na kuweka Saini Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki. Aldha, Vlongozi hao walizitaka Nchi Wanachama kukamilisha taratibu za kuridhia Itifaki hiyo ifikapo mwezi Julai, 2014.

Mheshimiwa Spika, manufaa ya Umoja wa Fedha ni pamoja na: kupunguza gharama ya kufanya biashara katika Nchi Wanachama; kuwezesha Nchi Wanachama kuwa na kiwango kidogo na tulivu cha Mfumuko wa Bei; kuwa na viwango vidogo vya riba ya kukopa; na kupusha athari za ubadilishaji wa fedha ndani ya Jumuiya kwa kuwa na Sarafu Moja. Matarajio ni kujenga ukanda tulivu wa kifedha (*Monetary and Financial Stability Zone*) utakaorahisisha na kusaidia ukuaji wa biashara na shughuli za kiuchumi ndani ya Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huo wa Kampala Wakuu wa Nchi pia waliridhia Mfumo wa kuanzisha Himaya Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuagiza kuwa ifikapo mwezi Januari, 2014, Nchi Wanachama ziwe zimeanza utekelezaji wake na kuukamilisha ifikapo au kabla ya mwezi Juni, 2014. Vile vile Wakuu wa Nchi walipokea Taarifa kuhusu maendeleo ya Mpango Kazi wa kuelekea kuanzisha Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Walitumia muda wa Mkutano huo kujadili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

hali ya usalama iliyopo katika nchi hizo na waliona kuna umuhimu wa kuongeza juhudini katika kukabiliana na Ugaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Mkutano huo ulikuwa na mafanikio mazuri na viongozi walitumia muda wao vilevile kubadilishana mawazo juu ya mambo mengine yanayohusu ushirikiano baina ya nchi hizo za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuhitimisha Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge hili, nilieleza kuhusu Programu ya Kuboresha Miji nchini (*Urban Local Government Strengthening Programme - ULGSP*) ya miaka mitano na leo naomba niseme maendeleo ya mradi huo ili Waheshimiwa Wabunge mwendelee kusaidiana na Halmashauri zetu kujaribu kusimamia jambo hili vizuri.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwendelezo wa Programu ya Uendelezaji na Uboreshaji Miji Nchini ambao kwa sasa unakaribia kumalizika utekelezaji wake. Programu hii ya kuendeleza Miji yetu hapa Tanzania ambapo sasa inahusisha Manispaa 11 na Miji 7. Manispaa hizo ni Tabora, Morogoro, Shinyanga, Lindi, Sumbawanga, Musoma, Songea, Singida, Iringa, Bukoba na Moshi. Miji mingine inayohusika ni Kibaha, Geita, Babati, Korogwe, Mpanda, Njombe na Bariadi. Halmashauri hizi zinazojumuisha Manispaa na Miji 18 na ziko tayari baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee juu ya vigezo hivi kwa sababu madhara yake visipotimizwa ni makubwa sana kwa miradi hiyo yote.

- i. Kuongeza Bajeti ya mapato kila mwaka;
- ii. Kutokuwa na Hati Chafu za Hesabu za Halmashauri;
- iii. Kuunda Kamati za kushughulikia matatizo yanayotokana na Programu kwenye ngazi ya Halmashauri, ngazi ya Kata na Mitaa;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

- iv. Kuhakikisha Programu hiyo imetangazwa na kueleweka na wakazi wa Halmashauri za Manispaa na Miji;
 - v. Kuhakikisha kuna Wakuu wa Idara wa kutoshaa;
 - vi. Kuhakikisha Sheria za Manunuzi zinafuatwa;
 - vii. Kuhakikisha Watu watakoahamishwa na Programu na kulipwa fidia hawazidi nyumba 20;
 - viii. Kuhakikisha miradi iliyotekelawa inalingana na thamani ya fedha iliyotumika;
 - ix. Kutekeleza miradi ya miundombinu iliyoko kwenye maeneo hayo;
 - x. Kupeleka taarifa za kila robo mwaka za miradi kwa muda unaotakiwa;
 - xi. Kuhakikisha kuna *Master Plan* ya Mji;
 - xii. Kuhakikisha ukusanyaji wa kodi ya majengo unaongezeka katika asilimia 5 hadi 30; na
 - xiii. Kuhakikisha taarifa za Mkaguzi wa Ndani zinaenda kwenye vikao vya Halmashauri kila robo mwaka.
- Mheshimiwa Spika, ukikosa hapa fedha hizo zinasimama.

Mheshimiwa Spika, nimetaja baadhi ya vigezo kwani viko zaidi ya 200 na vinagusa kila Sekta ya Halmashauri. Upimaji wa vigezo vyote vitafanyika mara mbili kwa mwaka; na Halmashauri zitakazoshindwa kufikia Alama (*Marks*) 60 na kuendelea, watapunguziwa fedha za miradi yao. Hivyo, Mikoa na Mabaraza ya Madiwani lazima yahakikishe kuwa vigezo vyote vinasimamiwa na kutekelezwaa kikamilifu. Aidha, TAMISEMI wawachukulie hatua za kisheria wale wote

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

watakaozembea katika kutimiza vigezo hivi na kuathiri maendeleo ya wananchi bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, Programu hii ambayo ni ya kwanza katika Afrika itatumia Dola za Kimarekani 255, fedha ambazo ziliikuwa zitolewe mwezi Julai mwaka 2013, lakini kutokana na matatizo ya ubadhirifu yaliyojitekeza kwa Wasimamiaji wa fedha zilichelewa kutolewa. Hata hivyo, sasa zimetolewa na tunaowamba sasa wote washirikiane katika Halmashauri hizo zote kuhakikisha miradi hii yote inasimamiwa vizuri na kwa ufanisi mkubwa ili wananchi waweze kunufaika na utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo mtakumbuka, wakati wa majadiliano ya Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa, kwa mwaka 2011/2012, Waheshimiwa Wabunge walionesha masikitiko yao kwa vitendo vya ubadhirifu na ujisadi unaofanywa na baadhi ya Halmashauri nchini. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia mjadala huo wakisema kuwa Serikali imekuwa haichukui hatua dhidi ya Watumishi wanaofanya makosa katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba wale wote wanaobainika wanachukuliwa hatua stahiki. Ziko pia jitihada mbalimbali zinazoonesa namna Serikali inavyojitahidi kuboresha utendaji katika Serikali za Mitaa. Jitihada hizi zimedhihirishwa na Matokeo ya Taarifa za Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo yanaonesha kuongezeka kwa ubora wa Hati za Ukaguzi zinazotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzia mwaka 2000 hadi sasa.

Kwa mfano, mwaka 2000/2001 Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ulifanywa na Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali unaonesha kuwa Halmashauri zilizopata Hati safi ziliikuwa 16 sawa na Asilimia 14 ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Halmashauri zote. Aidha, idadi ya Halmashauri zilizopata Hati zeny Shaka ziliwa 23, sawa na asilimia 20 na Halmashauri zilizopata Hati Chafu ziliwa 75 sawa na asilimia 65 ya Halmashauri zote.

Mwaka 2005/2006 Idadi ya Halmashauri zilizopata Hati Safi iliongezeka hadi kufikia 53, sawa na 43% na Halmashauri zilizopata Hati zeny Shaka ziliwa 67, sawa na 54% na Halmashauri zeny Hati Chafu ziliwa Nne, sawa na 3%.

Mwaka 2011/2012 taarifa za Ukaguzi ziliimarika zaidi ambapo Halmashauri zilizopata Hati Safi zilliongezeka maradufu hadi kufikia 104, sawa na 78% na zilizopata Hati zeny Shaka ziliwa 29, sawa na 21% na hakukuwa na Halmashauri iliyopata Hati Chafu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi ni kubwa. Hivyo, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti na mapato na matumizi ya Serikali kwa nguvu zake zote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo zinazoonekana, napenda kuwahakikisha kwamba Watumishi waliohusika na ubadhirifu wa mali na fedha za Umma wamechukuliwa hatua mbalimbali katika kuhakikisha kwamba tunajenga nidhamu. Kutohana na hatua hizo kati ya mwaka 2011/2012 hadi Septemba, 2013 kama mfano, jumla ya Wakurugenzi 52, Wakuu wa Idara 65 na Watumishi wengine 749 wamechukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria kwa ubadhirifu wa fedha katika Halmashauri mbalimbali nchini. Hatua hizo za kinidhamu ziko katika makundi yafuatayo:-

- i) Waliofukuzwa kazi ni 232;
- ii) Waliosimamishwa kazi ni 186;
- iii) Waliovuliwa Madaraka ni 33;
- iv) Waliopunguziwa Mshahara ni (1);
- v) Walioshushwa Cheo ni 32;
- vi) Walipewa onyo ni 113;
- vii) Waliofikishwa Mahakamani ni 233; na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

viii) Waliofikishwa Polisi na TAKUKURU ni 36.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia eneo hili la matumizi kwa nguzu zake zote ili kulinda pesaza umma zisihujumiwe bila sababu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kubadili na kuweka Mfumo wa '*Lawson*' katika kila Halmashauri ili kumaliza tatizo la mishahara kwa Watumishi hewa yaani waliofariki, walioacha kazi au wastaaifu. Vilevile kuna Mfumo wa *Epicor 9.05* ambao huu na ule wa *Lawson* zinasaidia kudhibiti Bajeti za Mapato na Matumizi katika Halmashauri nchini. Vilevile tutaendelea kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya Mifumo hii. Tayari ziko dalili nzuri sana zinazoonesha kwamba matokeo ya mifumo hii yameanza kuzaa matunda. Imani yangu ni kwamba tukilisimamia vizuri jambo hill litaleta matokeo mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Tumekuwa na muda mzuri wa kujadili masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya nchi yetu hapa Bungeni kwa kipindi chetu tulichokuwa katika Mkutano huu. Napenda niwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu. Kipekee nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri. Niwashukuru Wenyevitii wa Bunge kwa kazi nzuri ya kuongoza Vikao vya Bunge lako Tukufu. Aidha, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao wakati wa Mkutano huu.

Namshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake wote pamoja na Wataalam wote wa Serikali na Taasisi zake ikijumuisha Taasisi za Sekta Binafsi, kwa misaada ya Kitaalam na huduma mbalimbali za kufanikisha Mkutano huu.

Niwashukuru pia Waandishi wa Habari kwa kazi nzuri walizofanya kuhakikisha kuwa taarifa za majadiliano na maamuzi mbalimbali ya hapa Bungeni zinawafikia wananchi.

Niwashukuru Madereva kwa kazi nzuri waliofanya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

ya kuwasafirisha kwa usalama Waheshimiwa Wabunge, Viongozi mbalimbali, Wataalam na Wasaidizi wote walioshiriki katika Mkutano huu. Kipekee, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Naibu Mawaziri, watendaji wote kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kusaidia jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Wabunge kutokana na mjadala uiliojitokeza hapa jana na hatimaye tukaumaliza vizuri. Kipekee, niwashukuru na kuwapongeza sana Mawaziri wote wanenambari waliona uzito wa jambo lenyewe na wakaridhia kubeba mzigo wa kuwajibika kwa mujibu wa taratibu za kisiasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunahitimisha shughuli za Bunge hili tukiwa tumbakiza siku chache kabla ya kufika Mwisho wa Mwaka huu 2013. Tunamwomba Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema atujalie katika siku hizi chache tuweze kusherehekea Sikukuu njema ya Krismas na tuvuke salama mwisho wa mwaka na kuingia Mwaka Mpya 2014 kwa amani na furaha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wote tunavyofahamu, tutakuwa na Bunge la Katiba litakalofanyika mapema mwakani na kwa tarehe itakavyopangwa. Kutokana na utaratibu huo ni dhahiri kwamba wengi wetu tutakutana wakati wa Bunge la Katiba. Nitumie fursa hii kuwatachia safari njema mnaporejea kwenye maeneo yenu na wengi wenu niwatakia mapumziko mema ya Sikukuu ya Krismas na Mwaka Mpya hadi tutakapokutana wakati wa Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi litakapokutana kwa Mkutano Maalum wa Kumi na Tano wa Bunge la Bajeti tarehe 6 Mei, 2014 saa 3.00 asubuhi katika Ukumbi huu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache. Kwanza, tukushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelezo yako ambayo yametupitisha katika mambo makubwa ambayo yanafanya katika nchi yetu. Pengine tushawishi ofisi yako iwe inachapisha vitabu nya namna hiyo watu waweze kuwa navyo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, pale juu tunaye mgeni Mama Tunu Pinda na msaidizi wake. Karibuni sana. (*Makofii*)

Jana ilikuwa tuwe na ile tafrija fupi. Sasa wataalam wa kuandaa tafrija waliwakaribisha wasanii, wachezaji wa *Stand up Comedians*. Yuko pale Ndugu Jacob Mwakamele ndiye Mkurugenzi, yuko Ndugu Haris J. Malongo, naye ni Mkurugenzi na yuko Ndugu Abdul Yussuf na Ndugu Raymond Mushi na Ndugu Emmanuel Mathias. Hawa ndiyo ilikuwa jana wawe washereheshaji wa shughuli yetu, lakini tulahirisha kutokana na maneno mazito yaliyokuwepo humu, tukashindwa kwenda huko. Tunawakaribisha na tutawatafuta tena. Ahsante sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, halafu mmeona pale kwenye *park* ya Spika, kuna *ambulance* mbili za Bunge, zitakuwa zinafanya kazi wakati sisi tuko hapa au Dar es Salaam. Kwa sababu tumeshapata matukio makubwa yaliyotokea hapa tukashindwa kuwa-*rush* watu wetu mahali pazuri kwa sababu tulikuwa hatuna vyombo. Uzuri wa *ambulance* zile zina *first aid* mle completely mpaka mgonjwa atakapofika maeneo anayopaswa. Mara nyingi tukiwa katika kikao kirefu namna hii wagonjwa wetu wengine wanatakiwa wawe *rushed* hospitali, inakuwa matatizo, huwezi kuwapakia kwenye magari ya kawaida. Kwa hiyo, magari yale mnayaona mkipita yako mawili. (*Makofii*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

{SPIKA}

Nimeona Waheshimiwa Wabunge, mmeshtuka sana mliposikia Mheshimiwa Waziri Mkuu akisema Bunge la Bajeti litaanza tarehe 6 Mei, 2014. Hiki kikao chetu cha mwisho kabla ya Bunge la Katiba, ambalo inategemewa tarehe atakayotaja Mheshimiwa Rais, katikati labda ya mwezi Februari ndio litaanza. Kwa hiyo, tutakwenda moja kwa moja mpaka Bunge la Bajeti litakapoanza tarehe 6 Mei, 2014 aliyotaja Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa tumeona kutakuwa na mabadiliko mengi sana mwaka huu wa 2014. Vikao vyetu katika mwanzo wa mwaka vitababaika sana.

Waheshimiwa Wabunge, mtakwenda nyumbani sasa, lakini tarehe 27 Januari, 2014 mpaka tarehe 8 Februari, 2014 tutafanya kazi ya kukagua Miradi ya Serikali. Maana yangu ni kwamba, Serikali mjiandae, hatutakuwa na muda ule wa kawaida ule wa zamani wa kuanzia mwezi Machi, itabidi tuanze tu tarehe 27 Feburari, muanze kuangalia miradi ambayo mlipewa fedha kipindi hiki, hata kutathmini kama ni asilimia ngapi mmeshafikia na asilimia ngapi bado, mnawenza kutathmini kwa sababu Waheshimiwa Wabunge watapita kukagua Miradi yao na wenyewe wataandaa ratiba zao.

Kwa hiyo, kati ya tarehe 27 Januari mpaka tarehe 8 Februari, 2014 tutakuwa na kazi ya kutathmini Miradi ambayo tulipa fedha kipindi hiki tunachomaliza. Kwa hiyo, kidogo tuko *tight*. Tunaomba msifike pale mkaanza kudharauliana huko. Kwa hiyo na watu wenu waambieni, hii ratiba ni muhimu sana. Kwa sababu *impression* mnayopata hapa ndio inayokwenda kwenye Bajeti. Kwa hiyo, msiwaachie wataalam peke yao Waheshimiwa, hakikisheni na ninyi mna hakika na habari zenyewe. Kwa sababu wakipita jamaa hawa, wakiweka *impression* mbaya kuitoa itakuwa siyo rahisi.

Kwa hiyo, ni vizuri mkang'ang'ania kuangalia hela tulizopewa zimetufikisha wapi na tumefanya nini na watakuwa wanaweza ku-*estimate* mpaka Januari ni asilimia ngapi ilitakiwa kufanyika kabla ya mwezi Juni.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Kwa hiyo, naomba sana hili suala mlizingatie, kwa sababu baada ya hapo ndiyo tutaingia Kikao cha Bunge la Katiba. Tutakwenda na Bunge la Katiba, utaratibu mwagine tutapanga baadaye tutakavyoona baada ya Bunge la Katiba maana yake inawezekana pia tukawahoji Mawaziri *in between* kati ya vipindi vile vya Bunge la Bajeti, kama tutakuwa na *Saturdays* na nini, Kamati zile zitaanza kuwahoji Mawaziri kwa sababu wa kwenda kwenye molongo ule wa Bunge la Bajeti. Kwa hiyo, tutakuwa na utaratibu usio wa kawaida.

Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba tukishirikiana hakuna kitakachoharibika, tutapata Bunge la Katiba, tutakwenda kwenye Bunge la Bajeti yetu. Kwa hiyo, tutakapofika mwishoni pengine lile suala la kujimwaga sana linaweza lisiwepo kwa sababu muda utakuwa mfupi. Sasa mtu anayetaka mambo yake ajiandae. Wenzetu Bunge la Uganda wanatumia dakika tatu tu kujadili. Kwa hiyo, nadhani itafika mahali hapa tutafanya hivyo maana tutakuwa na siku chache. Toka tarehe 6 Mei, mpaka 30 Juni, 2014 ni muda mfupi. Kwa hiyo, itabidi tuangalie na mabadiliko haya tutayaleta, tutawasiliana.

Waheshimiwa Wabunge, la muhimu hapa ni kwamba, mnaondoka kwenda kwenye Majimbo yenu kwa muda wa wiki mbili au tatu tu, itabidi mrudi kufanya kazi tena kwa ajili ya kufidia kipindi ambacho tutakuwa tunatumia kwa ajili ya Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba pia nami niwashukuru sana. Bunge hili lilikuwa la moto moto hapa mwishoni, lakini ndivyo itakavyokuwa siku zijazo. Kwa sababu ile *element* ya kuwa na Vikao vya Taarifa za Kamati, lazima zitaibua maneno tu. Hatupendi kabisa kuona Mawaziri wanaondoka kila lakini ni dalili kwamba ni lazima kuwe na mabadiliko, na wala msishaachie Watendaji wenu tu, kwa sababu hawa jamaa watafanya hivyo kila mwaka kwa sababu kila mwaka watatoa taarifa. Ille nyngine tuliyosema habari ya *watchdog committees*, ule utaratibu wote mkiufuata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

mtakuta kuna hoja nyingine zitakuwa hazipo. Mkiufuta kabisa mpaka mkapata *treasury observation minutes* zikaletwa mtakuta kuna mambo mengine yamepungua. Mkiacha hivi hivi kweli itaondoa watu kila mwaka, kwa sababu tuna utaratibu wa Taarifa za Kamati.

Kwa hiyo, nisingependa iwe hivi, ningependa tubadiliike na tuonekane tunabadilika. Tukifanya hivyo hakuna ugomvi na mtu yejote. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa shughuli zote hizi na niwatakie Krismas njema na heri ya mwaka mpya mpaka tutakapoonana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nawahoji kuhusu Hotuba ya Waziri Mkuu aliyosema kwamba ataahirisha Bunge mpaka Tarehe 6 Mei, 2014. (*Makofi*)

*(Hoja illtolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Wallimba
Wimbo wa Taifa)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha Bunge mpaka tarehe 6 Mei, 2014 hapa hapa Dodoma.

(Saa 6.14 mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 6 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)